# Nipashe

Ijumaa Januari 5, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581546

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




UKURASA 21

**MBAPPE : SIJAAMUA HATIMA YANGU PSG**

**Mabosi** wa mikoa,ma-DED kitanzini miundombinu ya shule isiyokamilika UK. 5

**Karume** ataja siri wawekezaj kukimbilia Zanzibar UKURASA 17



**Israel** rasmi kortini UN mauaji Gaza UKURASA 19

## MKUTANO VYAMA VYA SIASA

# Watofautiana wakurugenzi kusimamia uchaguzi ujao

UK. 2



Baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa wakiwa katika ukumbi wa mikutano wa Mwalimu Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam walipohudhuria Mkutano Maalum wa Baraza la Vyama vya Siasa unaoshirikisha wadau wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa kujadili miswada ya sheria za uchaguzi na sheria za vyama vya siasa. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## YALIYOMO

UKURASA WA 24

**BENCHIKHA KICHEKO KIWANGO SIMBA SC**



WAKATI leo inawakabili APR FC katika mechi ya mwisho ya hatua ya makundi kwenye mashindano ya Kombe la Mapinduzi, Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, amesema kikosi chake kinaendelea...

**Kizimbani kwa mashtaka ya kumwingilia mbuzi**

UKURASA 3

## KIFO MTAALAMU HOSPITALI

# Familia yalalama kuambulia patupu

• **NI** aliyefariki akitibu wagonjwa wa marburg, mwanawe alia 'mkopo kiduchu' chuo kikuu, mjane ... *Endelea Ukurasa 4*

**MICHEZO** MAUYA AFUNGUKA, YANGA IKITOA DOZI UK.24

**MAONI** UK.6

# Watofautiana wakurugenzi kusimamia uchaguzi

**Na Mwandishi Wetu**



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko akizungumza wakati akifunga Mkutano Maalum wa Baraza la Vyama vya Siasa nchini ulioshirikisha wadau wa Demokrasia ya Vyama vingi Jijini Dar es Salaam jana .**PICHA: JUMANNE JUMA**

WADAU wa demokrasia na vyama vya siasa, wametofautiana kuhusu wakurugenzi wa halmashauri kusimamia uchaguzi na muundo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Wadau hao walitoa maoni kinzani wakati wakijadili muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi wa Mwaka 2023 na Muswada wa Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2023 kwenye mkutano maalum wa Baraza la Vyama vya Siasa jijini Dar es Salaam.

Mchambuzi wa masuala ya siasa, Deus Kibamba, alisema suala la wakurugenzi wa halmashauri kusimamia na kuratibu uchaguzi halina tatizo kwenye muswada kwa kuwa unaruhusu tume kuacha wakurugenzi na kuteua watumishi wengine wa umma.

"Ikitokea akateuliwa mtumishi, mkurugenzi hatajishughulisha na shughuli zozote za uchaguzi. Nimesisitiza kwa sababu kwa muswada huu, uchaguzi unaweza kusimamiwa bila wakurugenzi,"alisema.

Pia alishauri suala la teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kusisitizwa kwenye muswada kwamba itumike kila eneo linalowezekana.

"Vijana hawataki waache kazi zao waende kujiandikisha, Tume iandae programu atamizi (APP) ili kurahisisha uandikishaji wapigakura. Hii itapunguza foleni wakati wa uandikishaji au uboreshaji wa daftari la wapigakura," alisema.

Mwenyekiti wa Baraza la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGO), Dk. Lilian Badi, alisema suala la wakurugenzi halmashauri kuendelea kuwa wasimamizi wa uchaguzi ni muhimu kuzingatiwa kwa kuwa wana uelewa wa kutosha wa maeneo ya utawala ambayo shughuli za uchaguzi zitakuwa zinafanyika.

"Wadau wamezungumzia kesi ya Bob Chacha Wangwe. Mimi ningeshauri tukasome tufanye rejea vizuri. Sidhani kama tuna uelewa sahihi wa kesi hii. Kuteuliwa na Rais hakutawafanya wasitekeleze majukumu yao ipasavyo.

"Kesi haikusema wakurugenzi wa halmashauri hawaondolewi uhuru wa kuhudumu katika uchaguzi. Athari ambazo watu wako nje ya serikali kusimamia uchaguzi ni kubwa. Tuangalie pia gharama na watakuja kwa miezi mitatu serikali itaingia gharama kubwa sana katika kuwajengea uwezo wa kusimamia uchaguzi," alisema.

Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, alisema: "Ukisikia maelezo ya Deus (Kibamba) unaweza kulainika kwamba kifungu cha sita kiko vizuri. Ukisoma vizuri kina changamoto. Kimewataja wakurugenzi wa halmashauri kama lazima kusimamia uchaguzi."

Ili kuondoa malalamiko, alipendekeza kifungu kisomeke: 'Kwa madhumuni ya uchaguzi utakaofanyika chini ya sheria hii, Tume ya Uchaguzi itateua wasimamizi wa uchaguzi kuendesha uchaguzi katika jimbo au kata na msimamizi huyo anaweza kuwa msimamizi wa uchaguzi katika jimbo zaidi ya moja.

"Tusitaje cheo yaani tutaje mamlaka ya Tume kuteua. Pia kifungu cha 6 (2) kiboreshwe iandikwe: "Tume inaweza kuteua kwa kuzingatia nafasi aliyo nayo mtu katika ofisi au kwa jina kutoka miongoni mwa watumishi wa umma au Mtanzania yeyote mwenye sifa sawa zitakazotajwa katika kifungu cha 6(4) cha sheria hii wakurugenzi wa uchaguzi au wasimamizi wa uchaguzi kwa madhumuni ya kuendesha uchaguzi."

Alishauri kiongezwe kifungu kitakachotaja sifa za wasimamizi wa uchaguzi badala ya kutaja vyeo na itaondoa mgogoro wa namna ya kupata wasimamizi wa uchaguzi.

Kuhusu muundo wa Tume, Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, alisema katika kamati ya usaili Mkurugenzi wa Tume hawezi kuwa ndiye katibu wa kamati hiyo na kupendekeza kunahitajika kiongozi wa kamati awe mtu mwingine sio mtendaji wa Tume.

"Katika sheria ya Tume ya Uchaguzi iwe na watendaji wake katika kamati ya Usaili Mkurugenzi hawezi kuwa Katibu wa Kamati inayokwenda kuteua mabosi wake,"alisema.

Mwandishi wa Sheria, Thabit Mlangi, alipendekeza kuwa Mkurugenzi wa Tume waendelee kuchukuliwa watumishi walioko serikalini kwa kuwa ni mtu ambaye amefanyiwa usaili na kupekuliwa.

Dk. Mrisho Malipula, mhadhiri wa Chuo Kikuu Mzumbe, alisema dhana ya kupunguza mamlaka ya Rais katika kupata wajumbe na kuwapo kwa usaili kwa wajumbe ni mwanzo wa uhuru kwenye demokrasia.

"Tunaweza kujadili usaili uweje na sifa katika kuwapata wajumbe wa Tume, lakini kupunguza mamlaka ya Rais ni mwanzo wa kuwa na tume iliyobora zaidi tuboreshe ili tupate kitu kizuri zaidi," alisema.

**UWT NA USAWA**

Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Mary Chatanda, alisema sheria itamke wazi na wanapendekeza nafasi ya Mwenyekiti wa Tume na Makamu wake kuwapo na usawa wa kijinsia kama mwenyekiti mwanaume basi mwanamke awe makamu.

Mwenyekiti wa Ngome ya Wazee ACT-Wazalendo, Yassin Mohamed, alisema wazee hawajatajwa kwenye sheria zote za masuala ya siasa na uchaguzi na kwamba kwa kufanya hivyo hawatendewi haki.

Baruani Mshale kutoka Taasisi ya Twaweza, alisema kama hakutakuwa na tume huru utekelezaji wa sheria uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ukipitishwa bado haitawezekana kutekelezeka kwa kuwa kero nyingi zilizojitokeza kwenye uchaguzi uliopita, zilitokana na Tume kutokuwa huru.

Alisema pendekezo la mtu aliyetiwa hatiani asipige kura linakiuka haki ya raia na mtu asizuiwe kugombea kwa sababu zinazorekebishika na vigezo pekee vya kumzuia viwe vya kikatiba.

**KAULI YA BITEKO**

Akifunga mkutano huo, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Madini, Dk. Doto Biteko, alisema wadau wametoa maoni yao kwa kuzingatia maslahi ya taifa.

"Sisi serikali katika mkutano huu ni kama wadau. Nichukue nafasi kuitikia wito wa Spika wa wadau kwenda kutoa maoni yenu bungeni. Maoni yenu sisi kama serikali tutazingatia lakini ni vyema kwenda bungeni kutoa maoni yenu kwa kamati," alisema.

Alisema waliyojadiliana ni mwendelezo wa kujenga maridhiano ambayo yameasisiwa na Rais Samia Suluhu Hassan.


Bank of India (Tanzania) Ltd. BOI

**APPOINTMENT OF INDEPENDENT NON EXECUTIVE DIRECTOR IN THE BOARD OF BANK OF INDIA (TANZANIA) LTD**

Bank of India is a Leading Public sector Bank in India and completed 117 years in 2023. It has network of over 5100 Branches in India and 45 Overseas Branch/Offices across the globe in all important centers. Bank of India (Tanzania) Ltd, is a fully owned subsidiary of Bank of India.

The Board of Directors of Bank of India (Tanzania) Ltd would like to invite applications from suitable candidates for the position of **INDEPENDENT NON-EXECUTIVE DIRECTOR.**

For full job description Please visit **www.boitanzania.co.tz** & Email your Application with CV and Certificates to **Boi.Tanzania@bankofindia.co.in OR**

Send Physical Application through below mentioned address:

**Bank of India (Tanzania) Ltd**
**Head Office**
**Human Resources Dept**
**P.O.Box 7581**
**Maktaba Square,Maktaba Street**
**Dar es Salaam**
**Tanzania**

21776301

**HABARI KITAIFA**



Diwani wa kata ya Sedeko wilaya ya Serengeti mkoani Mara, Raphael Matiko akizungumza kwenye mkutano wa kujadili mambo mbalimbali ya maendeleo uliofanyika katika kijiji cha Bonchugu juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kizimbani akishtakiwa kwa kumwingilia mbuzi

**Na Steven William,** MUHEZA

SELF Sauli (25), mkazi wa kijiji cha Kwemnyesi, tarafa ya Bwembwera, wilayani Muheza, mkoani Tanga, amefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Muheza, akikabiliwa na mashtaka ya kumwingilia mbuzi jike. Mshtakiwa huyo alisomewa mashtaka hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Godfrey Haule, ikidaiwa kitendo hicho ni kinyume cha Sheria ya Makosa ya Kujamiiana, iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2002.

Akisoma mashtaka hayo, Inspekta wa Polisi Michael Msangawale, aliyesaidiana na Inspekta Joseph Njama, alidai kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo Novemba 3, mwaka jana katika kijiji cha Kwemnyesi.

Ilidaiwa mahakamani huko kuwa, mshtakiwa huyo alitenda kitendo hicho dhidi ya mbuzi anayemilikiwa na Ally Kiseto, mkazi wa kijiji cha Kwemnyesi, wilayani Muheza.

Mshtakiwa huyo alikana kutenda kosa hilo na kudai kuwa alikuwa anafanya kazi ya kuchunga mbuzi kwa bosi wake huyo.

Alidai kuwa kinachojiri dhidi yake ni matokeo ya kumdai mshahara wa miezi sita bosi wake huyo, akitaja una thamani ya Sh. 600,000.

Hakimu Haule alisema dhamana iko wazi, lakini mshtakiwa alikosa mdhamini, hivyo kurudishwa rumande mpaka Januari 18, mwaka huu kesi hiyo itakapotajwa tena.

# Jela miaka 30 unyang'anyi kutumia silaha

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa Morogoro imewahukumu watu watatu, wakazi wa Dumila, Kilosa mkoani hapa kifungo cha miaka 30 jela kila mmoja kwa kosa la unyang'anyi wa kutumia silaha.

Waliohukumiwa kutumikia kifungo hicho ni Athuman Jeremiah (19), Shamte Abubakar (27) na Amos Ayubu (19).

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Mkazi, Livin Lyakinana, alisema washtakiwa hao wametiwa hatiani baada ya ushahidi wa upande wa Jamhuri kujitosheleza na kuonyesha kuwa ni wazoefu katika kutenda uhalifu wa aina hiyo kwa kuwa walishawahi kufanya tukio kama hilo katika kituo cha mafuta cha Happy Oil kilichoko Dumila na kuwajeruhi walinzi kwa kutumia silaha ya kienyeji aina ya gobole kisha kutoweka.

Hakimu Lyakinana alisema mahakama imeamua kuwapa adhabu hiyo ili iwe fundisho kwao na kwa wengine wenye tabia kama hizo.

Washtakiwa hao ambao wote ni wakulima, walidaiwa kutenda kosa hilo Mei 12, 2023 majira ya saa 10:00 usiku katika maeneo ya maegesho ya magari makubwa katika kijiji na kata ya Dumila.

Ilidaiwa mahakama hapo kuwa wakiwa na silaha ya jadi aina ya kisu, washtakiwa walimnyang'anya Sh. 50,000 dereva wa lori, Deus Innocent, lililokuwa limepaki kwenye maegesho ya magari pembeni ya barabara kuu ya Morogoro - Dodoma.

Washtakiwa walifikishwa mahakamani Juni 27, mwaka jana, baada ya mchakato mzima wa mashtaka kukamilika na kutokana na Ushahidi uliotolewa, walikutwa na hatia, hivyo kuhjukumiwa kifungo cha miaka 30 jela kila mmoja. Kutokana na uamuzi huo, mmoja wa wakazi wa Morogoro, Halfan Saidi, alisema hukumu kama hizo zikitolewa, zinaipa jamii imani na vyombo vya dola kwa sababu kama kuna vibaka wengine na wezi wanatoweka au kuacha baada ya kujifunza kutokana na hukumu ya wenzao.


Canara Bank (Tanzania) Ltd.

**PUBLICATION OF INTEREST RATES, FEES AND CHARGES**

**PURSUANT TO REGULATION 11 OF THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS DISCLOSURE REGULATION, 2014 AND REGULATION 40(3)(a) OF THE FINANCIAL CONSUMER**

| S/N | DESCRIPTION | | PROPOSED CHARGES TZS | USD |
|---|---|---|---|---|
| 1 | **Monthly Maintanance** | SA | 2,000.00 | 2 |
| | | CA | 6,000.00 | 4 |
| 2 | **Non Maintanance of Minimum Balance** | SA | 1,500.00 | 2 |
| | | CA | 4,000.00 | 4 |
| 3 | **Account Statement Charges** | SA-Monthly | - | 0 |
| | | SA-Interim | 1,500.00 per page | 1.5 per page |
| | | CA-Monthly | Free | Free |
| | | CA-Interim | 1,500.00 per page | 1.5 per page |
| 4 | **Cash withdrawal charges** | SA-Up 25M | Free | |
| | | SA-Over 25M | 0.26% | |
| | | SA-Up to $2K | | Free |
| | | SA-$2K-$5K | | 0.60% |
| | | SA-Over $5k | | 0.60% |
| | | CA-Up to 25 M | Free | |
| | | CA-Above 25M | 0.26% | |
| | | CA-Up to USD 5K | | Free |
| | | CA-$ 5K-$10K | | 0.60% |
| | | CA-Above $ 10K | | 0.60% |
| 5 | **Cash Deposit Charges** | SA-Up to 25M | Free | |
| | | SA-Over 25M | 0.22% | |
| | | SA-Up $5K | | Free |
| | | SA-Over $5K | | 0.50% |
| | | SA-small currency ($1 to $20) | | 10.00% Minimum charge $1 |
| | | CA-Up to 50M | Free | |
| | | CA-Over 50M | 0.22% | |
| | | CA-Up to $10K | | Free |
| | | CA-Over $10K | | 0.50% |
| | | CA-small currency ($1 to $20) | | 10.00% Minimum charge $1 |
| 6 | **Balance Confirmation Certificate** | SA | 12,800.00 | 10 |
| | | CA | 21,200.00 | 13 |
| 7 | **Account Closure Charges** | SA | 20,000.00 | 20 |
| | | CA | 50,000.00 | 50 |
| 8 | **Activation of Dormant Account** | SA | Free | Free |
| | | CA | Free | Free |
| 9 | **Stop Payment Charges** | SA | Free | Free |
| | | CA | 35,000.00 | 28 |
| 10 | **Cheque Return Charges/Dishonoured Cheque** | CA-Inward | 50,000.00 | 50 |
| | | CA-Outward | 50,000.00 | 50 |
| 11 | **Cheque Clearing Charges** | CA-Inward | 1,300.00 | 1 |
| | | CA-Outward | Free | Free |
| 12 | **Ledger folio charges per folio (40lines per folio)** | SA | Free | Free |
| | | CA | 6,000.00 | 4.00 |
| 13 | **Cheque book Charges** | CA-50 Leaves | 42,000.00 | 27 |
| 14 | **Mobile Banking** | | | |
| i | Withdrawal Charge | Upto 100,000 | 1,700.00 | N/A |
| | | 101,000 to 200,000 | 2,600.00 | N/A |
| | | 201,000 to 400,000 | 4,300.00 | N/A |
| | | 401,000 to 600,000 | 5,100.00 | N/A |
| | | 601,000 to 999,000 | 6,800.00 | N/A |
| ii | Funds Transfer/Mobile Wallet | Upto 100,000 | 500.00 | N/A |
| | | 101,000 to 250,000 | 900.00 | N/A |
| | | 251,000 to 500,000 | 1,700.00 | N/A |
| | | 501,000 to 1,000,000 | 4,300.00 | N/A |
| | | 1,001,000 TO 10 Mn | 8,500.00 | N/A |
| 15 | **Locker Rent-Yearly** | Small | 296,700.00 | N/A |
| | | Medium | 508,500.00 | N/A |
| | | Big | 635,600.00 | N/A |
| 16 | **Remittances** | | | |
| i | TISS | Any amount per 1 transfer | TZS 8,450.00 | TZS 8,450.00 Equivallent |
| ii | E Remittances | Upto USD 1000 or Eq. TZS | 17,000.00 | $ 9.00 |
| | | 1001 to 5000 | 20,400.00 | $ 11.00 |
| | | 5001 to 10000 | 40,700.00 | $ 22.00 |
| | | 10,001 and above | 84,800.00 | $ 43.00 |
| iii | Swift Outward | Upto 5,000 | NA | $ 39.00 |
| | | 5,001 to 10,000 | NA | $ 51.00 |
| | | above 10,000 | NA | $ 77.00 |
| iv | Swift Inward | Upto 5,000 | NA | $ 11.00 |
| | | 5,001 to 10,000 | NA | $ 16.00 |
| | | above 10,000 | NA | $ 26.00 |

| | |
|---|---|
| **HEAD TREASURY AND TRADE FINANCE** | **03-01-24** |
| **GM-CREDIT** | **03-01-24** |
| **DEPUTY CEO** | **03-01-24** |

| S/N | DESCRIPTION | | PROPOSED CHARGES TZS | USD |
|---|---|---|---|---|
| 17 | **Loan/Advances Related Charges** | | | |
| i | Processing Charges | Upto 5 Mio - | 21,200.00 | |
| | | 5Mio to 10 Mio - | 169,500.00 | |
| | | 10 Mio to 25mio - | 339,000.00 | |
| | | 25 mn to 500 mio - | 1.28% | |
| | | >500mio--* (*minimum 7.5mio) | 1.06% | |
| | | Upto 5,000 - | | $85.00 |
| | | 5000 to 10,000 - | | $170.00 |
| | | Upto 20,000 - | | $255.00 |
| | | 20,000 to 500,000 - | | 1.28% |
| | | >500,000--* (*minimum 7,500) | | 1.06% |
| ii | Documentation Charges | Upto 100 MILLION | FREE | |
| | | >100 Mio (-Min 300,000) | 0.26% | |
| | | Upto 50,000 | | FREE |
| | | >50,000 - (Min 150) | | 0.26% |
| iii | Upfront fee on Term Loan | Upto 5Mio - | 21,200.00 | |
| | | 5 Mio to 10 Mio - | 169,500.00 | |
| | | 10Mio 25mio - | 381,400.00 | |
| | | 25 mn to 500 mio - | 1.53% | |
| | | >500mio--* (*minimum 9mio) | 1.28% | |
| | | Upto 20,000 - | | $255.00 |
| | | 20,000 to 500,000 - | | 1.53% |
| | | >500,000--* (*minimum 9000) | | 1.28% |
| iv | Inspection Charges | Upto 100 Mio - | 21,200.00 | |
| | | >100 mio - | 42,400.00 | |
| | | Upto 50,000 | | $22.00 |
| | | >50,000 | | $43.00 |
| v | Credit Reference Report Charges | | 101,700.00 | $43.00 |
| vi | Pre-payment penalty | Calculated as %ge pre-paid amount in the case of takeover of liability by other bank/lenders | 2.00% | 2.00% |
| 18 | **Guarantees (Local & International)** | | | |
| i | Bonds & Guarantees | per quarter (Min TZS 75,000) | 1.02% | 1.02% |
| ii | Bonds & Guarantees with 100 % Cash Margin | per quarter (Min TZS 75,000) | 0.43% | 0.43% |
| 19 | **Letter of Credit** | | | |
| 19.1 | **Import Letter of Credit (per qrtr of Part thereof)** | | | |
| i | Opening commission | commission Min $ 200 | NA | |
| ii | LC amendment Commission | Commision Min $50 max 350 | NA | 1.02% |
| iii | Swift charge for LC opening | | NA | 0.34% |
| iv | Swift charge for other message/amendments | | NA | $34.00 |
| v | Extensions - Commissions | commission Min $ 200 | NA | $34.00 |
| vi | LC cancellation charges | commission Min $ 200 | NA | 1.02% |
| vii | Non payment of Bills on due date | Till Payment | NA | 1.02% |
| 19.2 | **Export Letters of Credit (per quarter or part thereof)** | | | |
| i | Advising commission | | NA | $119.00 |
| ii | Confirmation Commission | Commision Min $150 | NA | 0.43% |
| iii | Negotiating bills under LC | Commision Min $75+cuourier+interest | NA | 0.43% |
| iv | Reimbursement claim paid | Commision Min $75 | NA | 0.43% |
| v | Commissions | Commision Min $200 | NA | 1.02% |
| vi | Collection of Export LC | Commision Min $75+cuourier+interest | NA | 0.43% |
| vii | Amendments | | NA | $64.00 |
| 20 | **Other disclosures** | | | |
| i | Base or Prime Lending Rate | | 16% | 10% |
| ii | Maximum spread above Base or Prime Lending | | 5% | 5% |
| iii | Penal Interest | | | |
| | a.For non compliance on Terms of Saction | Rate per year over regular rate of interest | 3% | 3% |
| | b.For Overdrawing/Excess drawing due to non payment of interest/installment/charges | Rate per year over regular rate of interest | 5% | 5% |
| vi | Deposit Rates | | | |
| | a. Current account | | Nill | Nill |
| | b. Savings bank deposit | | 3.00% | 1.00% |
| | C. Fixed Deposits Rates | **Up to TZS 50 M(up to USD 50,000)** | | |
| | | 30 -90days | 3.50% | 1.50% |
| | | 91-180days | 4.50% | 2.25% |
| | | 181-364 days | 5.50% | 3.00% |
| | | 1 year and above | 8.00% | 3.75% |
| | | 2 Years and Above | 8.00% | 4.00% |
| | | **TZS 50 M-100M (USD 50,000 -USD 100,000)** | | |
| | | 30 -90days | 4.50% | 2.25% |
| | | 91-180days | 5.50% | 2.50% |
| | | 181-364 days | 7.00% | 3.50% |
| | | 1 year and above | 8.25% | 4.25% |
| | | 2 Years and Above | 9.00% | 4.75% |
| | | **Above 100 M(Above USD 100,000)** | | |
| | | 30 -90days | 5.50% | 2.50% |
| | | 91-180days | 6.50% | 3.25% |
| | | 181-364 days | 7.50% | 4.00% |
| | | 1 year and above | 8.50% | 4.75% |
| | | 2 Years and Above | 9.50% | 5.00% |

# Familia yalalama kuambulia patupu

Na Romana Mallya

## -Ni aliyefariki akitibu wagonjwa wa marburg
## -Mtoto wake alia 'mkopo kiduchu' elimu ya juu
## -Mjane: Ahadi ya waziri, pensheni nazo kimya



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu.



Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul Badru.

FIKIRIA kuhusu watoto wanne (watatu wa kike) wa Amos Ernest, mtaalamu katika Kituo cha Afya Maruku, wilayani Bukoba, aliyefariki dunia Machi 15, mwaka jana kutokana na ugonjwa wa Marburg mkoani Kagera:

Mtoto wake mkubwa, Asumpta Kashumuni, binti mwenye umri wa miaka 19, mwishoni mwa mwaka jana alijiunga na Chuo Kikuu cha Kampala, jijini Dar es Salaam kusomea Shahada ya Maabara, fani ya baba yake, akiwa na simulizi ngumu kufikia mkopo wa elimu ya juu unaomwezesha kusoma.

Ni safari ndefu, alikwama mara tatu kupata mkopo huo, hata katika kile kinachotajwa amefanikiwa baadaye kwa kukata rufani, bado ni 'kiduchu' kulinganishwa na mahitaji kamili ya ada. Kwa kifupi, bado ana safari ndefu kukamilisha mahitaji.

Wadogo zake wawili kwa mama yao; anayemfuata anaingia kidato cha pili Jumatatu ijayo na wa mwisho anaingia darasa la pili. Wana ndugu yao mwingine, msichana toka kwa mama mwingine, anayeingia kidato cha kwanza mwaka huu.

Mama yao, Neema Njwelige, mkazi wa kata ya Izimbya, wilayani Bukoba, anabainisha kuwa baada ya kifo cha mumewe, aliyekuwa mtaalamu wa maabara katika Kituo cha Afya cha Maruku, maisha yao yamekuwa magumu kiasi cha kutokuwa na uhakika wa kupata milo yote kwa siku.

Neema anasema kuwa baada ya mumewe kufariki dunia kwa ugonjwa huo wa mlipuko, serikali kupitia Wizara ya Afya aliahidi kumsaidia katika maelezi ya watoto wake.

Anasema kuwa wakati anafariki dunia, mtoto wake wa kwanza alikuwa kidato cha sita na alikuwa anasoma chini ya ufadhili wa shirika la White Lake Enhancement and Education Transformation.

"Kwa sasa binti yangu wa kwanza yuko chuo kikuu na mtihani ninaopata ni hali ngumu ya maisha na mimi ni mama wa nyumbani. Nilimtegemea mume wangu kwa kila kitu," anasema.

Neema anasema kuwa baada ya mumewe kufariki dunia, fedha ambazo alipewa kama rambirambi ndizo zilimsaidia kuendesha maisha.

"Ninamshukuru Mungu mtoto wangu amechaguliwa kujiunga Chuo Kikuu cha Kampala, lakini nina changamoto kubwa ya ulipaji wa ada ambayo kwa mwaka ninatakiwa kulipa Sh. milioni 3.8.

"Kwa sasa mtoto ndio kwanza ameanza mwaka wa kwanza na nilichofanikiwa kulipa ni Sh. 950,000 tu kati ya Sh. milioni 3.8 zinazohitajika (kwa ajili ya ada ya chuo kwa mwaka). Ninaomba serikali isaidie kumpa mkopo," Neema anawasilisha kilio chake.

Mjane huyo anasema kuwa mtoto wake alipochaguliwa kujiunga chuo kikuu, aliufuata uongozi wa Wilaya ya Bukoba kuulizia ahadi iliyotolewa na serikali, lakini mrejesho ukawa kwamba lipo nje ya uwezo wao.

"Nilijaribu kumtafuta Waziri wa Afya (Ummy Mwalimu) aliyeahidi, lakini sikufanikiwa kumpata. Nikamtafuta Naibu Waziri (Dk. Godwin Mollel), nikaongea naye, akanitaka nimtumie taarifa za mtoto, nilifanya hivyo, lakini baada ya muda nilipomtafuta hakupokea tena simu.

"Mtoto wangu anachukua Shahada ya Maabara, ninaomba apate mkopo utakaomwezesha kuniondolea ugumu mimi, nina mzigo mzito tangu mume wangu afariki (dunia). Yeye ndiye alikuwa kila kitu katika familia," anasema.

Neema anasema mumewe alifanya kazi maabara kwa miaka 15 hadi umauti ulipomkuta.

"Ninaendelea kufuatilia fedha za mume wangu (pensheni) ingawa huko nako ninaambiwa si nyingi kulingana na miaka yake kazini na nimeambia muda wa kuzipata bado, hivyo ninaendelea kusubiri," anabainisha.

### MTIHANI KWA BINTI

Asumpta anayeanza kwa kurejea historia ya masomo yake, anasema kuwa baada ya kuhitimu kidato cha sita mwaka jana, alijiunga na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa mujibu wa sheria. Nyumbani mjomba wake alikuwa anaendelea na mchakato wa kumwombea nafasi ya kujiunga chuo kikuu.

"Awamu ya kwanza niliomba mkopo wa elimu ya juu sikupata. Ya pili na ya tatu sikupata, ikabidi nikate rufani lakini napo nikakosa na upande wa chuo chaguo la kwanza nilikosa, la pili nikakosa, chaguo la tatu nikachanganya kozi tofauti nikakosa.

"Nilipoweka vyuo binafsi ndipo nikapata vyuo vitatu; St. John, St, Joseph na Kampala, nikaamua kuja hapa Chuo Kikuu cha Kampala, nikiamini nitapata mkopo kwa kozi niliyochagua ambayo ni Shahada ya Maabara," anasimulia. Mwezi uliopita, serikali kupitia Wizara ya Afya iliwataka vijana wenye sifa za kusoma masuala ya tiba, wasomee kozi kama ya Asumpta kwa kuwa imenunua vifaa tiba vingi, lakini wataalamu wa eneo hilo ni wachache.

Asumpta anasema alipoingia chuoni huko aliamini angepata mkopo kwa kuwa utaratibu wa chuo hicho mwanafunzi anapoingia, anatakiwa kulipa walau asilimia 50 ya ada ya muhula mmoja (Sh. milioni 1.9).

"(Ada ya) nusu muhula ni Sh. 950,000. Wiki moja kabla ya mtihani wa muhula wa kwanza nikaona nimekosa kila kitu, nikaona niahirishe mtihani, ikabidi nimpigie mama, ilikuwa Novemba mwaka jana.

"Kitendo hiki kilimuumiza mama, akaamua kuhangaika anakojua, akanitumia Sh. 950,000 nikafanya mtihani. Hapa nina mtihani mwingine mwezi Machi, ninatakiwa nilipe Sh. 475,000," anasema.

Asumpta ambaye uso wake umekosa tabasamu, anasema, "yanayoendelea, yananifanya niwaze sana, lakini nimechagua kujikaza ili kutomwonesha udhaifu huu mama yangu. Ninachokiangalia kwa sasa ni wadogo zangu ambao wote wanamtegemea mzazi ambaye hana kipato.

"Inaniumiza kichwa sana lakini inabidi nijitahidi kutazama kilichopo mbele na nimwachie Mungu. Mimi ni mzaliwa wa kwanza na nina wadogo zangu watatu, hivyo ninajifunza kuacha kumlalamikia mama kila wakati, ataona kama amepoteza."

Mwandishi wa habari hizi jana alimtafuta Mkuu wa Mawasiliano wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Omega Ngole, ambaye baada ya mazungumzo, alipakua mifumo yao na kuthibitisha mwanafunzi huyo sasa ni mnufaika wa mikopo yao.

"Ninaomba umtafute huyo mwanafunzi umwulize kama ameshaangalia akaunti yake," Ngole alisema.

Nipashe iliporejea kwa Asumpta, mnufaika hiyo, baada ya kuingia katika akaunti yake ya HESLB, alibaini amepangiwa mkopo, lakini ni kwa vipengele viwili tu kati ya sita.

Vipengele alivyopatiwa mkopo ni posho ya kujikimu Sh. milioni 3.08 na ada ya chuo Sh. 420,000. Hajapangiwa mkopo katika vipengele vya mafunzo kwa vitendo, utafiti, posho maalum ya kitivo na posho ya vitabu na mahitaji ya darasani.

Kwa HESLB kumpangia mkopo wa Sh. 420,000, ina maana kwamba amepewa mkopo wa asilimia 11 ya ada ya chuo hicho ambayo ni Sh. milioni 3.8 kwa mwaka.

Kwa hesabu rahisi, mama yake ambaye ni mjane atapaswa kulipa kila mwaka Sh. 3380,000 kwa ajili ya ada ya chuo.

Awali, Ngole, akifafanua kuhusu mkopo aliopata mwanafunzi huyo, aliweka wazi kuwa kwa mwaka huu wa masomo, hakuna mwanafunzi aliyepatiwa mkopo wa asilimia 100 kwa vipengele vyote.

Alisisitiza kwamba, mtoto aliyepoteza wazazi wote huzingatiwa zaidi katika kupatiwa mkopo sawa aliyepata ufadhili wa msikiti au kanisa wakati wa masomo yake ya sekondari, pia wanafunzi wenye ulemavu.

Ngole pia alimtaka Asumpta kuandika barua kwenda kwa Mkurugenzi Mtendaji wa HELSB kama hajaridhika na kile alichopangiwa katika mkopo wake wa elimu ya juu.

### MeLSAT WALONGA

Rais wa Chama cha Wanasayansi Wanataaluma ya Maabara ya Afya Tanzania (MeLSAT), Yahya Mnung'a, alipotafutwa na mwandishi jana kuzungumzia kilichomsibu mwenzao Ernest, alisema:

"Hakuna fidia. Kilichopo ni kile kinacholipwa kwa mujibu wa OSHA (Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi) -- kwamba mtu mwenye mafunzo maalum, akipata janga kazini, analipwa fidia.

"Kilichotokea kwa mwenzetu kule Bukoba, tutakaa na mwanasheria ili atushauri twende vipi katika mazingira ya aina hii."

### WIZARA YA AFYA

Englibert Kayombo, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikali Wizara ya Afya, alipotafutwa na mwandishi jana mchana kuzungumzia madai ya mjane Neema dhidi ya wizara hiyo, aliomba atumiwe maelezo kwa njia ya maandishi ili aliwasilishe suala hilo kwa uongozi wa wizara.

Alipotafutwa tena na mwandishi jana saa 11:53 jioni, Kayombo alidai alikuwa kwenye kikao, akiahidi kutoa mrejesho baadaye, lakini hakufanya hivyo hadi tunaingia mtamboni.

## CMA yaagizwa kufanya utatuzi migogoro kazini

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imeagiza Tume ya Usuluhushi na Uamuzi (CMA) kuhakikisha inafanya utatuzi wa migogoro mahali pa kazi kwa haki na wakati ili kuvutia wawekezaji waweze kusaidia kukuza uchumi wa taifa.

Imesema CMA ni lazima ijitengenezee mazingira ya kuaminiwa na wananchi, wafanyakazi, waajiri na wawekezaji kwa kutenda haki ambayo itaonekana kwa pande zote mbili.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Profesa Joyce Ndalichako, alisema hayo wakati akifungua kikao kazi cha CMA chenye lengo la kufanya tathmini ya utendaji wa kazi na mafunzo yanayofanyika mjini Morogoro.

Prof. Ndalichako alisema CMA inapaswa kutenda haki hizo ili kupunguza kesi zinazopelekwa juu kwa majaji kutokana na baadhi ya wateja wao kukosa imani.

"Ifike wakati sasa kama CMA chombo ambacho kimeanzishwa kwa mujibu wa sheria tupunguze kesi zinazopelekwa kwa Jaji sio tutoe haki tu, lakini lazima ionekane haki imetendeka kwa pande zote mbili," alisema.

Alisema tume hiyo imeaminiwa na serikali kuleta mchango mkubwa na kasi ya kuongeza wawekezaji katika sekta binafsi na iwapo itatenda haki baina ya pande mbili kati ya mwajiri na mwajiriwa uwekezaji utaongezeka nchini.

Awali, Mkurugenzi wa CMA, Usekelage Mpulla, alisema katika utatuzi wa migogro ya kikazi, tume hiyo katika kipindi cha robo ya pili ya mwaka 2023/24 ilikuwa na migogoro 4,579 ya kikazi 1,859 iliyovuka mwaka na migogoro 2,720 iliyosajiliwa ngazi ya usuluhishi na uamuzi.

Alisema hadi kufikia robo ya pili ya 2023 jumla ya migogoro 2,712 sawa na asilimia 59 ya migogoro ya kikazi ilivuka mwaka na iliyosajili mwaka 2023/24 ilitatuliwa.

Mkurugenzi huyo alizitaja sababu zinazoongoza migogoro ya kikazi zipo tisa ambazo masuala ya ubaguzi, kusimamishwa kazi, kujengewa mazingira ya kuacha kazi, madhira, mikataba kuvunjwa isivyo halali, kutolipwa mishahara au kulipwa chini ya kima cha chini, haki za kichama, maombi/tafsiri/sheria.

Naye Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi, Dk. Yose Mlyambina, alisema mahakama hiyo inayohudumia mikoa ya Dar es Salaam na Pwani iliitisha majalada 350 kati ya hayo 313 yaliwasilishwa mahakamani kwa wakati 37 hayakuwasilishwa.

# Ma-RC, ma-DED kikaangoni ujenzi miundombinu ya elimu

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

KATIBU Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Adolf Ndunguru, amesema viongozi wa mikoa na halmashauri ambazo ujenzi wa miundombinu ya shule haujakamilika, waanze kujitafakari kabla ya kuchukuliwa hatua za kinidhamu.

Ndunguru alielekeza hayo jana alipofungua kikao kazi cha Makatibu Tawala Wasaidizi Elimu Mikoa na Maofisa Elimu wa Halmashauri nchini kinachofanyika mjini hapa.

Alisema licha ya dhamira njema ya serikali kutekeleza miradi mbalimbali ya elimu, baadhi ya viongozi wameshindwa kuisimamia na kukamilisha katika muda uliopangwa.

Katibu Mkuu alitoa mfano kuwa kuna mikoa ambayo ujenzi wa miundombinu bado uko chini ya asilimia 50 licha ya maelekezo ya serikali ya kuwataka kukamilisha kabla ya Desemba 30, mwaka jana.

Ndunguru alisema kumekuwapo visingizio na maelezo kadhaa kuhusu changamoto za kutokamilishaji kazi hiyo, akionya kuwa hayawezi kusaidia kwa wakati huu.

"Lazima mjue kuna waliokamilisha miradi hiyo huku wakiwa na mazingira magumu kuliko ninyi mnaosuasua.

Katika hili nikiwa ofisa nidhamu na ajira kwenu, sitaona haya kuchukua hatua dhidi ya wale wanaotukwamisha katika ukamilishaji wa ujenzi wa miundombinu ya shule pamoja na afua zingine za miradi," alionya.

Ndunguru aliwaagiza makatibu tawala wasaidizi elimu mikoa kusimamia kikamilifu ufundishaji na ujifunzaji shuleni ikiwamo kuhakikisha walimu wasiotimiza wajibu wao wanachukuliwa hatua stahiki.

Sambamba na hilo, aliwataka kuhakikisha wanafunzi wote wa darasa la tatu na kidato cha kwanza wanamudu stadi za lugha ya Kiingereza ifikapo mwishoni mwa mwaka.

Pia aliagiza kila halmashauri nchini kusimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo endelevu ya walimu kazini (MEWAKA) na kuhakikisha mafunzo hayo yanachangia ufanisi katika ufundishaji na uendelezaji.

Ndunguru aliwataka makatibu tawala wasaidizi na maofisa elimu wa halmashauri kuwahudumia walimu kwa upendo na kuwasaidia kutatua changamoto zinazowakabili.

Vilevile, aliwasisitiza kujenga tabia ya kuwatia moyo walimu na kusikilizwa badala ya kuwakatisha tamaa, ikiwamo kuacha kutumia lugha za udhalilishaji.

Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI anayeshughulikia Elimu, Dk. Charles Msonde, alisema utekelezaji mkakati wa uboreshaji elimu umeanza kuzaa matunda kwa kuonesha takwimu za watoto waliopimwa kila robo mwaka, akisema kuwa Machi 2023 kwa darasa la kwanza walijua kusoma, kuandika na kuhesabu.

## NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD, TRUST RECOVERIES LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| KIJITONYAMA | NEZAK INVESTMENT LTD | 1.NYUMBA YENYE HATI NA. DSMT1019002 KIWANJA NAMBA P23439 KIFURU-KINYEREZI 2. NYUMBA YENYE HATI NA. 70437 KIWANJA NA. '213', KITALU '14' BUNJU KINONDONI | 1. ZACHARIA ANTHONY KAPAMA 2. DAFROSA ATHONY KAPAMA | 1.KIFURU KINYEREZI-ILALA 2.BUNJU KINONDONI | 17/01/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | WAWA COMPANY LIMITED | 1.NYUMBA YENYE HATI NA. 115345, KIWANJA NAMBA 124, KITALU '24' KIBADA KIGAMBONI 2.NYUMBA YENYE HATI NA. DSMT1002975 KIWANJA NA. 2483, KITALU 'A' MBEZI MANYEMA 3.NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.KND/KGG/KATI/214 KIGOGO KATI 4. NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOPO | 1.SALUM JUMA NYANDOTO 2. SALUMU JUMA NYANDOTO 3.SALUM JUMA MARWA 4.SALUMU JUMA NYANDOTO | 1.KIBADA- KIGAMBONI 2.MBEZI MANYEMA 3.KIGOGO KATI 4.KINZUDI GOBA | 19/01/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MAIN | TOMONI FARMS LIMITED | SHAMBA LENYE HATI YA MAUZIANO YA SERIKALI YA KIJIJI, EKARI 194 | FRANKLIN G. BAGALLA | KIJIJI CHA TOMONI-KIBITI RUFIJI | 18/01/2024 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KARIAKOO | LAMECK JOHN RUGIGA | 1.NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO 2.NYUMBA YENYE HATI MILIKI NA.59847 KIWANJA NA.2009 KITALU ''D'' | 1.LAMECK JOHN RUGIGA 2.CRISPIN PATRICK KAPILIMBA | 1.MBEZI MSHIKAMANO 2.SINZA | 19/01/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KIJITONYAMA | HP PLANNERS & EVENTS MANAGEMENT LTD | NYUMBA (2) | 1.JAMES NDASKOI NNKO 2.DAPHROSER ABEID HAMZA | 1.TEGETA 2.KIGAMBONI | 24/01/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | VICTOR STEVEN MANG'ANA | NYUMBA | VICTOR STEVEN MANG'ANA | UKONGA | 18/01/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | KOKUBELWA PAUL NGAMBEKI | KIWANJA | ANTHONY AARON ICHWEKELEZA | MPIJI MAGOE | 19/01/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | BAHATI YOHANA NYATO | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | BAHATI YOHANA NYATO | LYAMKENA-MAKAMBAKO | 19/01/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | FRENK SAMSON LEMAU | NYUMBA ZENYE HATI YA MAUZIANO | FRENK SAMSON LEMAU | SHEWA-MBEYA | 15/01/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | NYUMBA (2) ZENYE HATI MILIKI | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | 1.MBEYA MJINI 2. TUNDUMA | 16/01/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | VENANCE JISKAKA MWAKYABALA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | VENANCE JISKAKA MWAKYABALA | MWANJELWA , MBEYA MJINI | 16/01/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | EMANUEL MOYO MASETA | 1.NYUMBA (3) 2.KIWANJA | EMANUEL MOYO MASETA | 1.IFWEKENYE -MBOZI 2.SONGWE | 23/01/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | NDIMBWELU BANDEKISYE KAFWENDA | NYUMBA | PAULO KALOTA NDAWILA | NZOVWE-MBEYA | 18/01/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | IPYANA TIGER JUNIOR | NYUMBA | IPYANA TIGER JUNIOR | ILEMI-MBEYA | 15/01/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | BRAITON REBEN MWANKEMWA | NYUMBA | BRAITON REBEN MWANKEMWA | IVUMWE | 24/01/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | IDD SALUMU HUSSEIN | NYUMBA | EDITH JOSEPH CHIWAMILA | ISYESYE | 24/01/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | CHARLES JOHN ZIMBA | NYUMBA | CHARLES JOHN ZIMBA | ITEZI -MASHARIKI | 17/01/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | PRIVA EMANUEL SHIRIMA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | PRIVA EMANUEL SHIRIMA | KITETE-MBEYA | 11/01/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | MARIAM BATON MWANDENENE | NYUMBA | VUMILIA ELIAS NYAGAWA | NGOSI- MWAKIBITI | 19/01/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | OWDEN MKUMBALA NYONDO | NYUMBA | OWDEN MKUMBALA NYONDO | ISYESYE-MBEYA | 19/01/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | WILLY MWITIKA MGOGO | NYUMBA | WILLY MWITIKA MGOGO | MLOWO-MBEYA | 23/01/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | GRACE ADONIAS MTEGO | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.22 KITALU 'N' HATI NA.4870 | BLASIUS SWAI KAGINA | BUNDA | 23/01/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | ABAS HAMAD ISSA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | PETER NDULU MAHARAGE | MISUNGWI-MWANZA | 17/01/2024 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MARIA JOHN PETRO | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | JOHN PETRO KALISA | KILOLELI 'B' - MWANZA | 23/01/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | 1.NYUMBA 2. KIWANJA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | 1.IGELEGELE BUGARIKA 2. BUJINGWA-MWANZA | 18/01/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | SELEMANI CHARLES MNIKO | NYUMBA | SELEMANI CHARLES MNIKO | MBUGANI -MWANZA | 19/01/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | JOSEPH MAKALA MAKALA | NYUMBA | JOSEPH MAKALA MAKALA | NYASAKA ILEMELA MWANZA | 23/01/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | JAMES JACOB KALULEMA | NYUMBA | JAMES JACOB KALULEMA | MAHINA KANYERERE-MWANZA | 23/01/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBAGALA | NORBERT LUDOVICK KWIYAKA | NYUMBA | NORBERT LUDOVICK KWIYAKA | CHAMAZI DOVYA | 10/01/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KINONDONI | VAM COMPANY LIMITED | NYUMBA | VENANT ANGELO BAKEMYA | BUNJU | 16/01/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | HASSAN RAMADHANI SHEKIKA | NYUMBA (2) | 1.HASSAN RAMADHANI HARASHI 2.HASSAN RAMADHANI SHEKIKA | 1.YOMBO DOVYA-MAKANGARAWE 2.TAMBANI MKURANGA | 25/01/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | SEGUMBA JAPHAR MHANDO | NYUMBA | SEGUMBA JAPHAR MHANDO | VIWEGE-MAJOHE | 08/02/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | DEVOTA JOHN KATINDASA | NYUMBA | MASOUD HAMAD SEIF | KICHANGANI- MAJOHE | 29/02/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | MHINA JOSEPH KWELLA | NYUMBA | MHINA JOSEPH KWELLA | PUGU | 18/01/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | CHACHA ITEMBE NYAMAISA | NYUMBA | SHAABAN SHILLINDE BULILO | NYAMHONGOLO | 19/01/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | NCHAMA SKANIA MANGORYO | NYUMBA | NCHAMA SKANIA MANGORYO | MKOLANI MWANZA CITY | 22/01/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | ALOYCE ALOYCE KIMARO | NYUMBA | YAHAYA HUSSEIN ATHUMAN | PASIANSI MWANZA | 19/01/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | MARIANA BENEDICT MASSAWE | NYUMBA | SHIJA DAUDI NDUNGILE | ZENZE - ILEMELA | 23/01/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | FAUSTINE KISYERI MAIHA | NYUMBA | DEUSDEDIT NYANDA MIKOMANGWA | NYAMANORO - MWANZA | 24/01/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | SIKITU HAMIS YAHAYA | NYUMBA | HAJI ABEID KASUBI | NYASAKA ILEMELA MWANZA | 18/01/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0715868000/0714939933/0785242219/0759282344/0787129539/0767808848/0754497396/0678799566
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ubunifu wa kutangaza utalii Kagera uigwe mikoa mingine

**TANZANIA** imejaliwa kuwa na vivutio vya utalii katika maeneo mbalimbali ambavyo huchangia kwa kiasi kikubwa katika pato la taifa. Kutokana na vivutio hivyo, watalii huingia nchini kila mwaka kwa ajili ya kutembelea maeneo hayo na kwa kufanya hivyo, hulipa fedha ambazo huingia katika mfuko wa serikali kwa ajili ya maendeleo ya sekta za kiuchumi na kijamii.

Pamoja na kuwa na vivutio hivyo vya utalii, ni mikoa michache tu ambayo watalii hufika hususan ile ya kaskazini kwenye mbuga za wanyama, Zanzibar na Nyanda za Juu Kusini. Mikoa mingine licha ya kuwa na vivutio ni nadra kupata watalii.

Kwa kutambau umuhimu wa sekta hiyo na kujitangaza kitaifa na kimataifa, mkoa wa Kagera umeandaa programu maalumu ya kutangaza utalii. Mbinu iliyotumika ni ya wasanii 100 wa kada tofauti kuzuru mkoani humo mwezi ujao kwa lengo la kutangaza vivutio vya utalii vilivyoko.

Mpango huo ni mkakati uliotokana na ziara ya mmiliki wa kampuni ya Sepenga Entertainment, Goodhope Ntimba, maarufu kama Madam Sepenga, mkoani humo na kubaini una vivutio vingi vya utalii. Pamoja na kubaini wingi wa vivutio hivyo, alishangaa ni kwa nini havitangazwi ndipo akachukua jukumu la kufanya hivyo.

Ziara hiyo ya wasanii iliyopewa jina la Grand Kagera Tour, itahusisha pia wasanii wa kada ya uigizaji ambao wanatarajiwa kuandaa igizo litakaloonyeshwa kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, lenye maudhui ya mila na desturi za wakazi wa Kagera.

Kwa ujumla Kagera ina historia kongwe ndani ya taifa la Tanzania hasa machifu wa zamani kabla ya ujio wa wakoloni na ni sehemu ambayo ilikuwa ya mwanzo kwa wamisionari kufika na kueneza Ukristo. Kutokana na historia hiyo, Kagera ina vivutio vinavyojumuisha mabaki ya mapango yaliyokuwa yanatumiwa na machifu; watu walikuwa wanayatumia kuabudu na kufanya ibada za mavuno.

Pia Kagera ni sehemu ambayo ilivamiwa na Nduli Idi Amini mwaka 1978 na kutokana na hali hiyo, kuna baadhi ya majengo ambayo yaliharibiwa kwa mabomu na yamebaki magofu, hivyo yakitangazwa yanaweza kujulikana na kuvutia watalii. Kwa hakika ziara hiyo itakayofanyika kwa siku 28, itaibua mambo mengi na iwapo yatatangazwa kikamilifu, utalii ndani ya mkoa huo utakuwa sehemu ya kuungizia mkoa mapato na taifa kwa ujumla.

Wazo lililoibuliwa la kutangaza vivutio vya utalii katika mkoa wa Kagera linapaswa kupongezwa kwa kuwa si tu litaibua vitu vitakavyochangia kukua kwa uchumi bali linaamsha ari ya watu kupenda sehemu walizotoka na kuziendeleza. Kama ilivyo Kilimanjaro, wananchi wanaotoka Kagera kwa sehemu kubwa wamewekeza makazi ya kudumu na wamekuwa wakijivunia kwa kufanya hivyo.

Kwa mantiki hiyo, Watanzania wengine wafuate nyayo za Kagera kupitia mbunifu huyo kutangaza vivutio katika mikoa yao ambavyo vitawezesha watalii kufika na kuchangia fedha ambazo zitaingia katika mkondo wa kiuchumi.


Rais Samia Suluhu Hassan baada ya kuingia tu madarakani, alibaini kuwa Tanzania ina vivutio vingi vya utalii, hivyo kuamua kucheza filamu ya The Royal Tour ambayo imeipaisha nchi katika medani ya kimataifa. Matokeo ya filamu hiyo yanaonekana kutokana na idadi kubwa ya watalii kuingia nchini.

Ni vyema ubunifu uliofanywa kwa Kagera ukaigwa na watu wa mikoa mingine ambao pia ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za Rais Samia kutangaza utalii nchini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Halfani Chusi

# Juhudi za kudhibiti ajali, kipengele dhidi ya uchovu wa dereva muhimu

**NI** miaka mingi sasa kumekuwapo mikasa kadhaa, ambayo ajali ya barabarani inapotokea, sababu kuu inaangukia uzembe wa dereva uliosababishwa na usingizi au uchovu.

Hapo ndipo inaonyesha haja ya serikali na mamlaka husika kuwekeza zaidi nguvu kupunguza ajali zinazotokana na visababishi hivyo.

Kwa sasa serikali kupitia Jeshi la Polisi, limeupiga mwingi kwa kuwa na kifaa kinachoweza kupima kiasi cha kilevi kwa dereva, vivyo hivyo kuwapo pia kupima uchovu.

Kwa hakika, teknolojia ya kupima kilevi imesababisha kupungua kwa ajali zitokanazo na ulevi, wahusika wakiogopa kuendesha chombo cha moto kwamba watatambuliwa.

Hata hivyo, kipo kisababishi kingine cha ajali ambacho ni uchovu kwa dereva na hii mara nyingi hutokana na dereva mmoja kuendesha umbali mrefu bila kupumzika au kupokelewa.

Uchovu ni chanzo kikubwa cha ajali za barabarani. Uchovu huu huweza kusababishwa na vitu vingi ikiwamo, kufanya kazi kwa muda mrefu bila kupumzika.

**Uchovu ni chanzo kikubwa cha ajali za barabarani. Uchovu huu huweza kusababishwa na vitu vingi ikiwamo, kufanya kazi kwa muda mrefu bila kupumzika.**

Pia, kufanya kwa muda mrefu shughuli inayotumia akili sana, kutopumzika vya kutosha, kuwa na msongo wa mawazo, au mchanganyiko wa vyote kwa pamoja vilivyotajwa hapa.

Kwa ujumla wake, uchovu huweza kusababisha lolote kwenye shughuli yoyote inayohitaji umakini kuitimiza kwake ikiwamo udereva miongoni mwa madhara yanayoweza kutokea inaweza kuwa

Kutoona vizuri, kuathiri uwezo wa kufanya maamuzi sahihi, kufanya vitendo ambavyo vinakiuka kanuni za kuendesha gari, mfano kubadili gia au kupunguza mwendo, kwa mazoea tu bila ya kujitambua.

Mambo hayo nayo yanaathiri uwezo wa kupangilia mambo, kupunguza umakini, kuondosha hali ya kukaa kwa tahadhari, kupunguza au kuondosha uwezo wa kukumbuka vitu ambavyo tayari umeshavifanya, kuona, au kusikia.

Ni mambo yanayosababisha mtu afanye makosa madogo madogo mara kwa mara, na kama ni barabarani ananusurika mara nyingi kupata ajali.

Hali ya kushindwa kuitikia kwa haraka vichocheo au mabadiliko ya ghafla ya mazingira au hali ya kushindwa kuwa na mantiki na maamuzi, ikiwamo kufanya maamuzi ambayo katika hali ya kawaida, usingeyafanya, mfano 'ku-ovateki' pasipowezekana, kunaathiri uwezo wa kuwasiliana.

Wapo madereva wanaotumia vinywaji kama kahawa na kilevi aina ya mirungi kuondoa usingizi wanapokuwa barabarani, lakini ukweli ni kwamba dawa ya kupunguza uchovu ni kulala.

Shida ya madereva wanaoendesha gari umbali mrefu bila ya kupokezana na wengine, nayo huwafikisha mahali wanachoka maarafu na kujikuta wanaelemewa na usingizi, hivyo kuhatarisha usalama wake na watumiaji wengine wa barabara.

Ipo haja, ya kuangalia namna ya kupambana na suala la uchovu kwa madereva wa magari yanayokwenda umbali mrefu kwa kuweka sheria kali na kiwango cha umbali ambacho dereva anatakiwa kupumzika.

Serikali na wamiliki wa magari wote kwa pamoja wawe na lengo moja, watimizie wajibu wao hii itaondoa ajali zinazotokana na uchovu kwa madereva.

Japo ipo shida kwamba wamiliki wengi wa magari hawapendi kuajiri madereva wawili kwa ajili ya kuepuka gharama za kuwalipa kwamba akiwa nao atawalipa fedha nyingi bila kukumbuka anapokuwa mmoja akichoka anaweza kusababisha ajali na kuharibu gari.

# Wanaokopesha bila leseni ya BoT kuchukuliwa hatua

**Na Jenifer Gilla**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) imeendelea kuonya kuwa itazichukulia hatua za kisheria taasisi, kampuni au watu binafsi wanaofanya biashara ya kukopesha fedha bila kuwa na leseni. Taarifa iliyotolewa na BoT juzi, kwa mara nyingine ilikumbusha wananchi kuwa ni kosa kwa taasisi, kampuni au watu binafsi kujihusisha na biashara ya kutoa mikopo bila leseni kwa mujibu wa Kifungu Na. 16 cha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018.

Kupitia taarifa yake hiyo, BoT ilitahadharisha wakopaji kuhusu mikataba wanayoingia na wakopeshaji, ikiwataka kuisoma, kuielewa na kukubaliana na vigezo na masharti ikiwamo gharama na masharti mengineyo ya mikopo hiyo.

"Tunasisitiza kuwa mkopeshaji anatakiwa kutoa nakala ya mkataba wa mkopo kwa mkopaji. Vilevile, mkopaji ana haki ya kudai na kupewa mkataba wa mkopo kila anapochukua mkopo," BoT ilifafanua katika taarifa yake hiyo.

Benki Kuu pia ilisisitiza wananchi kuepuka kukopa au kufanya biashara na taasisi, kampuni au mtu binafsi ambaye hana leseni kutoka BoT na kuwaelekeza kupekua tovuti ya benki hiyo kuhakiki uhalali wa taasisi hizo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, kuanzia mwezi huu, BoT itaanza kutumia mfumo unaotumia riba kutekeleza Sera ya Fedha badala ya kutumia mfumo unaotumia ujazi wa fedha.

Ilisema mabadiliko hayo yanalenga kuongeza uthabiti wa sera hiyo katika kudhibiti mfumuko wa bei na kuimarisha shughuli za kiuchumi.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, mabadiliko hayo ni utekelezaji makubaliano ya kutumia mfumo mmoja wa utekelezaji Sera ya Fedha ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na jumuiya nyinginezo za kiuchumi ambazo Tanzania ni mwanachama.

Kupitia mfumo huo, BoT itakuwa inatoa maelekezo ya riba itayotumika katika soko la fedha baina ya benki, itakayojulikana kama Riba ya Benki Kuu.

Katika taarifa hiyo, BoT ilifafanua kuwa mabadiliko ya utekelezaji wa sera hiyo kwa kutumia mfumo wa riba, hayana maana ya kuweka ukomo katika viwango vya riba zinazotozwa na benki na taasisi zingine za fedha nchini.

Kwa mujibu wa BoT, riba zinazotozwa na taasisi hizo, zitaendelea kuamuliwa na nguvu ya soko kuendana na sera zingine za kiuchumi nchini.

BoT ilianzishwa kisheria mwaka 1965, lakini ilianza kazi rasmi mnamo Juni 14, 1966, yaani miaka 57 iliyopita.

Hata hivyo, kwa sasa, BoT inaendesha shughuli zake kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya Mwaka 2006.

# Jafo aagiza miradi ikamilishwe kwa wakati

**Na Julieth Mkireri,** KISARAWE



MBUNGE wa Kisarawe, Dk. Selemani Jafo (pichani), amesema viongozi wanaotakiwa kusimamia miradi ya maendeleo, wanapaswa kuzingatia ukamilishaji miradi kwa wakati na kuondoa vikwazo kwa wananchi.

Amesema katika jimbo hilo mikakati yao inajumuisha utekelezaji wa maelekezo ya kisera; kila kijiji kuwa na zahanati ifikapo mwakani ili kuwaondolea adha wananchi wanaotembea umbali mrefu kupata huduma za afya.

Dk. Jafo ambaye pia ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), aliyasema hayo juzi alipozungumza na wananchi wa vijiji vya kata za Marui, Vikunburu na Chole alikokwenda kukagua miradi ya maendeleo.

Alisema miradi inayopelekwa kwa wananchi ikisimamiwa vizuri na viongozi kama ilivyopangwa, itaondoa vikwazo kwa jamii na wataendelea na shughuli zingine za maendeleo kuinua uchumi wao.

Katika utekelezaji miradi ya ujenzi wa zahanati ngazi ya vijiji, zaidi ya Sh. milioni 50 zimetolewa kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kujenga miradi hiyo. Kufikia Machi mwaka huu, baadhi ya zahanati zitakuwa zimeshaanza kutoa huduma.

"Nimetembelea miradi ya nyumba ya mwalimu katika Shule ya Msingi Ngongere na nimeelekeza kupitia fedha za Mfuko wa Jimbo ikamilike kwa wakati ili hawa walimu wapate sehemu ya kuishi," alisema.

Waziri Jafo alisema wataalamu wanatakiwa kubadilika na kuzingatia fedha zinazotengwa zinafika kwa wakati maeneo ya miradi ili wanufaika waondokane na vikwazo.

Alipongeza ujenzi wa Zahanati ya Mafumbi, kata ya Chole, akisema uongozi wa kijiji hicho ni mfano bora wa kuigwa kutokana na usimamizi wa miradi pindi wanapopewa fedha.

Jimbo la Kisarawe lina vijiji 76. Kati yake, vinane havijapata zahanati na hadi sasa, huku jimbo hilo likiwa na vituo vya afya vinane ambavyo vinatoa huduma ikiwamo ya upasuaji.

Sera ya Afya, Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya 2020-2025, vinaeleza serikali kuhakikisha kila kijiji kinakuwa na zanahati na kila kata iwe na kituo cha afya.

**Air Tanzania**
*The Wings of Kilimanjaro*

## VACANCY ANNOUNCEMENT

Air Tanzania Company Limited (ATCL) is expanding its network to meet the needs of its Business Strategy which focus on sustaining the recorded achievements and remain an airline of choice that meets and exceeds customers' expectations in line of its mission of provision of reliable, safe and high-quality services. Therefore, applications are invited from qualified Tanzanian to fill the position mentioned below:

**1. POSITION: SENIOR INSURANCE OFFICER (RISK MANAGEMENT) (1 POST)**

**1.1 QUALIFICATIONS**
- Must be holder of Bachelor Degree in one of the following fields; Insurance, Risk Management, Actuarial Science or relevant field from a recognized and reputable institution.
- Must have minimum of seven (7) years working experience in risk management field.

**1.2 RESPONSIBILITIES:**
i. Coordinate efforts for developing and enhancing appropriate risk management framework, procedures and systems in consultation with management.
ii. Coordinate and monitor the implementation of risk management initiatives within the Company.
iii. Work with risk owners to ensure that the risk management processes are implemented in accordance with agreed risk management framework and strategy.
iv. Collect and review all risk registers and their treatment plan for consistency and completeness.
v. Provide advice and tools to staff, management, Board and the Board Committees on risk management issues, including facilitating workshops in risk identification.
vi. Promote understanding of and support for risk management including delivery of risk management training.
vii. Oversee and update corporate risk register, with inputs from risk owners.
viii. Perform any other duties as assigned by the supervisor.

**2. POSITION: RECORDS MANAGEMENT ASSISTANT I (RE-ADVERTISEMENT) (1 POST)**

**2.1 QUALIFICATIONS**
- Must be a holder of Diploma in one of the following fields: Records Management, Records and Archives Management, Corporate Information Management, or equivalent qualification from recognized institutions.
- Must have working experience of at least four (4) years in related field.

**2.2 RESPONSIBILITIES:**
i. Ensure that a file register is in place.
ii. Receive incoming mail, stamp and record them in relevant register.
iii. Send mail preview box to preview officers and record daily movement of files
iv. Ensure letters have all attached documents referred to; and letters are signed by relevant desk officers after attending to them
v. Ensure that envelopes are affixed with proper stamps and are addressed correctly
vi. Circulate flimsy files to the authorized officers.
vii. Develop individual objectives/targets and performance standards as part of the individual performance agreement in consultation with the immediate superior.
viii. Perform any other official duties as provided by the supervisor.

**3. TERMS AND CONDITIONS:**
Ten (10) years contract with attractive remuneration and Fringe Benefits as per ATCL Salary Structure and Incentive Scheme.

**4. MODE OF APPLICATION:**

Interested applicants must submit a dully signed letter for consideration of the applications attached with the following:
i. A detailed curriculum vitae (CV);
ii. Certified copies of all certificates (including Secondary School and birth certificate), and other relevant certificates and licenses. (Applicants who have studied outside Tanzania should have their certificates approved by relevant authorities i.e. Tanzania Commission for Universities (TCU) or National Examination Council- NECTA)
iii. Two recent passport size photographs;
iv. Names and addresses of at least two reputable referees;
v. Applicant's reliable contact address, email address and telephone numbers.

**Note:** Misrepresentation of facts and qualifications during application shall warrant legal consequences. Previous applicants for the position of Record Management Assistant I may re-apply.

**5. CLOSING DATES:**
Applicants should reach the undersigned within 14 days from the first date of this announcement: -

**MANAGING DIRECTOR & CHIEF EXECUTIVE OFFICER**
**AIR TANZANIA COMPANY LIMITED,**
**P.O. BOX 543,**
**DAR ES SALAAM**
**Date: 5th January 2024**

***ATCL is an equal opportunity employer. Women are encouraged to apply. Misrepresentation of qualifications or any other information on application shall warrant legal consequences***

# Kairuki yasimika mtambo kuondoa uvimbe bila upasuaji

**Na Joseph Mwendapole**

HOSPITALI ya Kairuki ya Mikocheni jijini Dar es Salaam imeanza kutoa matibabu ya kuondoa uvimbe bila upasuaji kwa kutumia mtambo tiba unotumia mwangwi wa sauti (Ultrasound).

Mtambo huo High Intensity Focused Ultrasound (HIFU), unaweza kutibu uvimbe bila upasuaji.

Mtaalamu mwendeshaji wa mtambo huo, Dk. Fredy Rutachunzibwa, alisema unatibu uvimbe kwenye kizazi, figo kongosho, ini, mifupa, matiti na unaoweza kuonekana kwenye mtambo huo.

Alisema ulianza kufanyakazi Januari, mwaka huu na una uwezo wa kutibu hadi wagonjwa 10 kwa siku.

Alisema faida za tiba kwa kutumia mtambo huo mgonjwa hapati maumivu makali, anapata nafuu haraka, kutopoteza damu na kuepukana na makovu ya upasuaji.

Alisema tayari wagonjwa wanne wamefanyiwa matibabu hayo tangu kuwasili kwake na unatarajiwa kuzinduliwa rasmi hivi karibuni.

"Mtambo huu mbali na kuwa na uwezo huo utawanufaisha sana wanawake wenye kusumbuliwa na vimbe zinazosababisha changamoto za uzazi sasa vimbe zikiondolewa watapata ujauzito kwa urahisi," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Kairuki, Dk. Asser Mchomvu, alisema mtambo huo ni wa nne kwa Afrika na uko pia nchi za Misri, Afrika Kusini, Nigeria na sasa Tanzania kwenye hospitali hiyo.

Alisema hospitali hiyo imewapeleka nje ya nchi wataalamu wake wawili kupata mafunzo na wamemaliza na kubobea kuendesha mtambo huo.

"Uwezo wa mashine ni kutibu hadi wagonjwa 10 kwa siku ila inategemea aina ya vimbe aliyonayo mgonjwa. Kwasababu kuna mwingine anakuwa na vimbe hata nne," alisema.

"Zamani tulikuwa tunafanya upasuaji kwa kufungua tumbo, tukahamia kwenye njia ya upasuaji kwa kutumia matobo na sasa hivi tumeendelea zaidi tunatoa uvimbe huo huo bila kupasua wala kuweka matobo hiki nikiwango cha juu zaidi cha matibabu," alisema.

Dk. Mchomvu alisema hospitali hiyo imeunda timu maaalum ya kutibu bila kufanya upasuaji inayoitwa HIFU Kliniki itakayokuwa inaendeshwa na wataalamu wabobezi wa hospitali hiyo.



Mwenyekiti wa shirika la (ALALA) All for Love, Love for All, Manuel Le Nahedic, (katikati), akivishwa vazi la jadi na Mosse Laizer (kushoto) na Toima Makeseni, lililotolewa na wakazi wa Kitongoji cha Samanga Wilayani Simanjiro Mkoani Manyara, baada ya kufanikisha mradi wa awamu ya pili ya maji kutoka mlima Landanai na kujenga matenki mawili na birika ya kunyweshea mifugo juzi. **PICHA : GIFT THADEY**

# DAWASA kuwafikia wateja 20,000 Kibamba

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Majisafi ya Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), kupitia mkoa wa kihuduma Kibamba umejipanga kuwafikia wateja 20,000 mwaka huu kutoka 15,000.

Mamlaka hiyo imesema lengo lake ni kuwafikia wananchi wote wa eneo lake la kihuduma ifikapo mwaka 2025.

Ofisa Biashara wa mkoa wa DAWASA Kibamba, Ian Mlay alisema jana kuwa mikakati iliyopo ili kuwafikia wateja 5,000 zaidi ni pamoja na kufanya miradi midogo midogo ya kuwaunganishia wateja huduma baada ya kukamilisha miradi mikubwa ukiwamo wa maji mshikamano.

"Moja ya mpango wetu ni kuhakikisha tunawafikia wateja wote wa eneo tunalolihudumia kwa kuongeza wigo wa mtandao wetu wa huduma, tunawaomba wateja wetu wasisite kuleta maombi ya kuunganishwa na huduma zetu," alisema Mlay.

Pia alisema malengo mengine ni kupunguza idadi ya wateja wenye madeni ya muda mrefu kwa kuingia makubaliano maalum ili waweze kulipa huduma kidogo kidogo huku wakiendelea kupata maji.

"Tunaendelea kuwasihi wateja wetu kulipia huduma kwa wakati na kutosubiri kusitishiwa huduma ambapo ulipaji wa bili zetu kunachangia maendeleo kwa maeneo mengine ambayo bado hayajapata huduma," alisisitiza Mlay.

Aidha, alisema DAWASA Kibamba imejikita kuendeleza ushirikiano baina yake na wateja kwa kutoa elimu na taarifa mbalimbali kupitia makundi sogozi ikiwamo mitandao kwa Whatsapp, mitandao rasmi ya kijamii ya DAWASA na kituo cha huduma kwa wateja.

Alisema mkoa wa kihuduma Kibamba unahudumia kata tano za Msigani, Kwembe, Kiluvya, Kibamba na sehemu ya kata ya Mbezi na kwamba ofisi za DAWASA Kibamba zinapatikana eneo la Mbezi Luguruni karibu na ofisi ya Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo.

# Mwenyekiti ajeruhiwa visu akimkamata mtuhumiwa

**Na Samson Chacha,** TARIME

MWENYEKITI wa Kitongoji cha Gwitanka wilayani Tarime mkoani Mara, Michael Magasi, amejeruhiwa kwa kuchomwa visu mwilini wakati akijaribu kumkamata Sinda Meja anayetuhumiwa kudaiwa fedha katika kilabu cha pombe za kienyeji.

Ofisa Mtendaji wa kata hiyo, Wakuru Mirumbe alisema Januari 2, akiwa na wenzake walikuwa wanamsaka Meja ili wampeleke kwa mtendaji huyo ndipo ulipotokea ubishi na mtuhumiwa kumchoma Magasi visu ubavuni, mkononi na kwenye makalio hali iliyosababisha kuvuja damu nyingi.

Alisema wasamaria wema walimpa msaada wa kumkimbiza Hospitali ya Migori iliyo nchi jirani ya Kenya na kulazwa.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi, Mtendaji huyo alisema kuna maeneo katika mji wa Sirari yenye vibaka wanaopora watu mali yakiwamo ya Nyamorege, Sokoni, karibu na kanisa la SDA na kanisa Katoliki na machinjio mapya na baadhi yao wakitoka nchi jirani ya Kenya wakiungana na wa Sirari kufanya uhalifu.

"Tunawaasa Watanzania raia wema kuwa na mshikamano kuwafichua wahalifu wakamatwe na kufikishwa katika vyombo vya sheria ili wananchi waishi kwa amani," alisema.

Diwani wa Kata ya Sirari na viongozi wenzake, waliliomba Jeshi la Polisi kufanya msako wa pamoja katika maeneo yenye shida ya vibaka.

Kamanda wa mkoa wa Kipolisi Tarime Rorya, ACP Michael Njera, alithibitisha kutokea tukio hilo la kuchomwa visu mwenyekiti huyo na kwamba wanamsaka mtuhumiwa na kuwahimiza wananchi kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo kumkamata.

Alionya watu wote wanaotembea na silaha za jadi watakamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria kwa kuwa kutembea nazo bila kibali cha serikali ni kosa la jinai.



# Ukishusha, kupakia abiria stendi bubu 20,000/- itakuhusu

**Na Hamida Kamchalla,**
KOROGWE

HALMASHAURI ya Mji wa Korogwe mkoani Tanga, imepiga marufuku mabasi ya abiria yaendayo mikoani pamoja na mabasi madogo kushusha abiria katika stendi zisizo rasmi ama ofisi zao kwa kuwa ni kosa kisheria.

Badala yake imeelekeza kutumika kwa kituo kikuu cha mabasi cha serikali ambacho ni mahususi kwa wasafiri na wasafirishaji.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji huo, Tito Mganwa, aliyasema hayo jana na kueleza kuwa uamuzi huo unatokana na baadhi ya wasafirishaji kusababisha kero kwa abiria wanaokwenda maeneo ya vijijini.

Mganwa alisema ukaguzi wa mara kwa mara umekuwa ukifanyika ili kuona maeneo ambayo mabasi yanasimama kama yanaruhusiwa kupakia na kushusha abiria na yote hayo hufanyika kwa kuzingatia sheria za halmashauri ya mji huo.

"Kwa mujibu wa sheria ndogo za halmashauri yetu ni kosa kwa mtu kupakia au kushusha abiria nje ya stendi kubwa ya mjini humo ambayo ndio inayotambulika uwepo wake kisheria" alisema. Hata hivyo alisema katika kudhibiti vitendo hivyo vya kupakia na kushusha abiria kwenye vituo visivyo rasmi waliepuka kutokutumia nguvu na hivyo kuchukua hatua ya kuketi meza moja na wasafirishaji.

"Tukasema tusianze kutumia nguvu kutoza faini, tulianza kutoa elimu mwezi wa sita kwa madereva na wamiliki wa vyombo vya usafirishaji, tumetoa elimu Julai na Agosti," alisema. Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo baada ya kuona kwamba vitendo hivyo vinaendelea ndipo halmashauri ilipoanza kutekeleza sheria kwa kutoza faini kwa watu ambao wamekuwa wakikiuka makubaliano waliyowekeana.

Alisema kwa yoyote atakayekiuka atatozwa faini ya Sh. 200,000 kama kima cha chini na kisizidi Sh. milioni moja kama kima cha juu na kusema kuwa lengo siyo kuwakomoa wasafirishaji ila ni kuhakikisha watu wanafuata sheria zilizowekwa. "Azma yetu sio faini ila ni kuona watu wanafuata taratibu, faini hii ya Sh. 200,000i tumekuwa tukitoa muda wa siku saba mtu kulipa tangu alipokamatwa kwa sababu pengine wakati anakamatwa anakuwa hana" alisema. Aliongeza: "Vituo bubu ambavyo vimekuwa vikitumika kupakia na kushusha abiria siyo salama kwa abiria na hata watumiaji wengine wa miundombinu ya barabara katika wilaya yetu" alisema Mganwa.

Aliongeza kuwa Mji wa Korogwe una stendi yenye ubora na usalama kwa watumiaji wake na ndiyo inayopaswa kutumika, huku akibainisha kuwa sheria ya kutoza faini imeanza kutekelezwa kwa watu wanaootoa huduma kwenye sehemu zisizokuwa rasmi.



Mwanzilishi wa Maktaba Jamii ya Martha Onesmo, Jennifer Dickson, (mwenye kipaza sauti) akitoa maelezo jinsi maktaba hiyo itakavyohudumia wananchi kwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Profesa Adolf Mkenda (katikati) na viongozi wengine wa Serikali na Dini wakati wa uzinduzi wa maktaba hiyo uliofanyika katika viwanja vya usharika wa Kisangeni, wilayani Mwanga mkoani Kilimanjaro jana.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kiteto yapata neema fedha mfuko wa jimbo

**Na Cynthia Mwilolezi,**
MANYARA

KATA 12 za Wilaya ya Kiteto mkoani Manyara zimenufaika na miradi ya maendeleo kupitia fedha za mfuko wa jimbo zilizotolewa na mbunge wa Kiteto, Edward Ole Lekaita.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Lekaita, alisema kata hizo zimenufaika na mfuko huo ambao umewagusa kulingana na mahitaji ya miradi yao.

"Wananchi wenzangu baada ya salamu za mwaka mpya, napenda kuwafahamisha kuwa kamati ya mfuko wa jimbo, ambayo ilikaa Desemba 28 mwaka jana iliweza kujadili maombi ya miradi ya wananchi kutoka kata 12 na baada ya kikao, kamati ilitenga fedha katika miradi hiyo,"alisema.

Alifafanua kuwa Kata ya Kibaya ilipatiwa Sh.milioni tano kwa ajili ya umaliziaji wa vyumba viwili vya madarasa, Shule ya Msingi Ngarenaro na Kata ya Kaloleni Sh.milioni tano kwa ajili ya utengenezaji wa madawati katika Shule ya Msingi Kaloleni na Kata ya Lengatei Sh.milioni sita kwa ajili ya umaliziaji wa vyumba viwili vya madarasa katika Shule ya Msingi Malimogo.

Vile vile alisema Kata ya Sunya Sh.milioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa Soko la Sunya, Kata ya Partimbo Sh.milioni tano kwa ajili ya utengenezaji viti na meza Shule ya Msingi Mbeli, Kata ya Chapakazi Sh.milioni sita kwa ajili ya kupaua vyumba viwili vya madarasa, Shule ya Msingi Osteti.

Aidha alisema miradi mingine ni fedha kwa ajili ya umaliziaji wa nyumba ya daktari wa Zahanati ya Ndaleta Kata Njoro ambayo ilipewa Sh.milioni sita na Kata ya Ndedo Sh.milioni tano kwa ajili ya utengenezaji wa madawati katika Shule ya Msingi Ngabolo na Kata ya Namelock Sh.milioni sita kwa ajili ya ukamilishwaji wa ujenzi madarasa mawili ya Shule Msingi Oloimug'i.

Pia alisema Kata ya Laiseri ilipata Sh.milioni sita kwa ajili ya ukamilishwaji wa ujenzi nyumba ya mwalimu katika Shule ya Msingi Kiteto, Kata ya Dosidosi zaidi ya Sh.milioni 6.5 ilipata kwa ajili ya kupaua nyumba ya daktari wa Zahanati ya Nchinila.

Pia Kata ya Loolera ilipata Sh.milioni tano kwa ajili ya umaliziaji wa nyumba ya waalimu wa Shule ya Msingi Lembapuli.

"Kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu, tunamshukuru sana serikali kwa kuendelea kuboresha maisha yetu wana Kiteto kwa kuendelea kutuletea miradi mikubwa ya maendeleo na kushughulikia changamoto za wananchi katika wilaya yetu.

"Kwa dhati kabisa nawahakikishia kuwa nitaendelea kuwa sauti yenu bungeni na kuwawakilisha ipasavyo kwa unyenyekevu na uaminifu mkubwa," alisema.

Hivyo, alitoa wito kwa watumishi wote na viongozi ngazi za vijiji na kata kuhakikisha miradi hiyo inasimamiwa vizuri na kwa ufanisi mkubwa ili wananchi wapate huduma hizo kwa wakati.

# Watendaji kata, mitaa watwishwa zigo usimamizi miradi

**Na Oscar Assenga,**TANGA

MKURUGENZI wa Jiji la Tanga, Said Majaliwa amewataka watendaji wa kata na mitaa kuhakikisha wanasimamia vema miradi inayotekelezwa katika kata zao.


Majaliwa aliyasema hayo jana wakati akizungumza na watendaji hao na kuwaagiza wasimamie vema miradi hiyo ili kuondokana na changamoto za miradi viporo.

Alisema licha ya maagizo hayo pia kwanapaswa uondokana na miradi iliyokaa muda mrefu bila kukamilika, huku akieleza kumekuwa na changamoto ya watendaji waliopewa miradi kutokufika mara kwa mara kuikagua.

Aidha alisema kitendo hicho cha watendaji kutokufika kukagua miradi waliokabidhiwa katika maeneo yao inasababisha kuchelewa kwa ukamilishwaji miradi kwa wakati.

Hata hivyo aliwataka watendaji wa kata na mitaa kusimamia mapato yote yanayokusanywa kwenye kata zao, kuhakikisha wanapata taarifa ya ukusanyaji wa mapato katika vyanzo .

alisema: "Lakini niwaombe watendaji kushirikiana katika kila changamoto wanayokutana nayo kwenye vyanzo hivyo kwa lengo la kuona namna nzuri ya kuzitatua".





# RC awataka waliojenga kando ya Ziwa Victoria kuondoka

**Na Vitus Audax,** MARA

WAKAZI wa Wilaya ya Musoma mkoani Mara waliojenga nyumba ndani ya mita 60 katika eneo oevu la Hifadhi ya Ziwa Victoria na Bwawa la Kitaji wametakiwa kuhama ili kuepusha madhara ya mvua na ongezeko la kina cha maji vinavyohatarisha maisha yao.

Hatua hiyo inakuja baada ya agizo la Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda juu ya watu wanaoishi katika maeneo ambayo hayajarasimishwa kuondolewa mara moja ili kudhibiti madhara ya mvua ambayo yamekuwa yakitokea kwa wananchi mkoani hapa. Akitekeleza agizo hilo juzi lililoenda sambamba na kuzibua mitaro na makaravati yaliyoziba ili kunusuru nyumba zaidi ya 70 zilizozingirwa na maji katika bwawa hilo, Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Halfan Haule alisema suluhisho la kudumu ni wote waliojenga kando ya ziwa waondoke haraka.

"Tunaendelea na jitihada za kuzibua mitaro lakini pia tunaangalia suluhu za kudumu juu ya tatizo hili ambazo ni pamoja na kujenga mtaro mkubwa utakaotoa maji mengi kutoka katika Bwawa la Kitaji pamoja na kuwasihi wananchi waliopo katika maeneo hatarishi kuhama," alisema.

Kaimu Meneja wa TARURA Wilaya ya Musoma, mhandisi Mohamed Atanga alisema kazi ya kuzibua mitaro inaendelea vizuri, huku akiwataka wananchi kuhifadhi mitaro kwa kutokutupa taka hovyo ili kuhakikisha inaendelea kutiririsha maji yake katika maeneo sahihi.

Katika hatua nyingine wananchi wa Kata ya Kitaji ambapo nyumba zao zimezingirwa na maji wamegoma kuhama katika maeneo hayo kwa kile kinachoelezwa kuwa hawana maeneo ya kwenda. Walisema licha ya hali kuendelea kuwa mbaya bado wanalazimika kuendelea kuishi na kulala katika nyumba hizo zilizojaa maji kutokana na kukosa maeneo mbadala pa kuhamia.

"Vyumba vyangu vitatu vyote bado vina maji licha ya kuwa katika siku tatu hizi maji yamepungua katika uwanja lakini tunatafuta njia mbadala kwa ajili ya kupita na kuingia ndani ambapo hata hivyo bidhaa na mali zetu zimezingirwa na maji," alisema Zubeda Khasim mkazi wa Kitagi

Diwani wa Kata ya Kitaji, Golden Charles alitaja kazi ya kuwaamisha wananchi katika maeneo hayo imekuwa ngumu kutokana na hali zao za kiuchumi.



Baadhi ya wazazi wakinunua mahitaji ya shule kwa ajili ya watoto wao wanaosoma ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya kufunguliwa kwa shule wiki ijayo. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# Waliouza pamba mwaka 2022/23 kujazwa mapesa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

CHAMA Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU) mkoani Shinyanga, kinatarajia kuwalipa wakulima wa pamba waliouza katika msimu wa mwaka 2022/2023.

Mwenyekiti wa chama hicho, Tano Nsabi aliyabainisha haya jana wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake juu ya namna walivyojipanga kukabiliana na mvua za El-Nino zisiharibu uzalishaji wa zao hilo pamoja na tumbaku.

Nsabi aliwasisitiza wakulima kuzingatia ushauri unaoendelea kutolewa na maaofisa kilimo ili kupata mavuno mengi kwani kwa msimu huu wanatarajia kununua zaidi ya kilo milioni 5.5 tofauti na msimu uliopita ambapo walinunua zaidi ya kilo milioni tatu.

"Watalaamu wetu wa fedha wanaendelea na kupiga hesabu zao kulingana na idadi ya wakulima waliotuuzia pamba ili kuangalia ni kiasi gani kinatarajia kulipwa watakapomaliza tutawalipa wakulima wetu malipo ya pili kupitia akaunti zao za benki, niwatake wawe wavumilivu malipo yao watayapata,"alisema Nsabi.

Alisema wameomba mkopo katika Benki ya Kilimo Tanzania (TADB) ili kuanzisha kiwanda cha kutengeneza mafuta ya kula yanayotokana na mbegu ya zao hilo hali itakayowaongezea mapato ya ndani kwenye ushirika na kulipa malipo ya pili kwa wakulima kiasi kizuri na chakuvutia uzalishaji kuongezeka.

Alisema watakapopata mkopo huo watanunua mashine yenye uwezo mkubwa wa kukamua mafuta yatakayotokana na mbegu, kuuza makapi na mashudu kwa wafugaji wa mifugo na kwamba eneo la kufunga kiwanda hicho lipo kwasababu eneo la ushiriki ni kubwa na linahitaji uwezeji wa namna hiyo.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Msingi Uyogo (AMCOS), Maganga Masanja alisema kwenye AMCOS kuna wakulima 257 wanaolima zao hilo.

Alisema msimu uliopita walifanikiwa kuzalisha tani 50 za pamba na kuuza kwa bei elekezi ilioyokuwa imepangwa na serikali ya Sh. 1,050 na KACU kununua pamba kulisababisha kuwepo kwa ushindani wa bei na kampuni nyingine na wakulima kupata fedha.

# Hospitali ya Uyui yapewa bil.2.6/- ununuzi vifaa tiba

**Na Halima Ikunji,** UYUI

HOSPITALI ya Wilaya ya Uyui mkoani Tabora imepatiwa zaidi ya Sh.bilioni 2.6 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba vya kisasa, ujenzi wa jengo la kisasa la kuhifadhia maiti pamoja na upasuaji.

Akizungumza na Nipashe juzi Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Tumaini Fumbuka alisema fedha hizo zilitolewa na serikali katika mwaka huu wa fedha 2023/24 kwa ajili ya kuwaondolea adha wananchi kufuata huduma hizo umbali wa zaidi ya kilomita saba.

Dk.Fumbuka alisema kwamba katika kipindi cha Novemba walipokea fedha nyingine kwa ajili ya miradi ya ujenzi wa vyoo ambavyo vitatumika kwa wagonjwa na matangi ya kuhifadhia maji.

Alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa jitihada zake za kuendelea kuboresha huduma katika hospitali hiyo ikiwemo kupelekewa vifaa vya kisasa vya miozi, ultrasound, vifaa vya tiba za meno na macho pamoja na vichomea taka.

Alitaja kupatikana kwa vifaa hivyo kuwa kumewasaidia kutoa huduma zilizobora ambazo hapo awali zilikuwa zinatolewa kwenye Hospital ya Rufani ya Kitete mkoani hapa.

Aidha alisema kutokana na maboresho yanayofanywa na Sserikali yamesaidia ongezeko la ajira pamoja na huduma bora na za karibu kwa wagonjwa kulinganisha na kipindi cha nyuma wananchi walikuwa wanafuata huduma hizo umbali mrefu na kutumia fedha nyingi kwa ajili ya kusafiri kufuata huduma.

Mkurungezi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Leokadia Humera alisema serikali imetoa fedha pia kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya hospital, vituo vya afya na zahanati 65 ambavyo vyote kwa sasa vinatoa huduma bora.

Humera alisema fedha hizo zimesaida kujengwa kwa majengo mbalimbali ikiwemo la kinamama kujifungulia, upasuaji, mionzi, maabara ya kisasa na jengo la kufulia nguo kwa ajili ya hospital hiyo.

Baadhi ya wananchi wa wilayani hapa akiwemo, Mariam Lushu alisema hospitali hiyo kwa sasa inatoa huduma bora tofauti na kipindi cha nyuma ambapo vifaa vilikuwa hakuna, hivyo kuomba serikali kuendelea kuboresha zaidi huduma hizo.




Msikilizeni mtaalamu Profesa Janabi anakufaeni sana, acheni hizo bezo!




**Dawa za kulevya zinavyotoboa mifuko maisha ya kila siku, wenye dhamana nao wakijipanga**

BUFE
IJUMAA JANUARI 5, 2024
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
Nipashe

2024 NA SIMULIZI INAWEZEKANA...

# Aliyenasa shule kwa mimba, yuko mlango wa pili kielimu na biashara

**Na Beatrice Philemon**



Susana Ng'ombe, akionyesha bidhaa ya jam aliyotengeneza baada ya kupata mafunzo kupitia programu ya DREAMS. **PICHA: BEATRIRCE PHILEMON.**

SUSANA Ng'ombe ni msichana wa miaka 23 anayeishi katika kata ya Mkwawa, DonBosco, mkoa wa Iringa, ambaye alishindwa kutimiza ndoto yake ya elimu, baada ya kupata mimba akiwa na umri wa miaka 17 mwaka 2019 akiwa kidato cha pili.

Baada ya kujifungua, wazazi wake wakashindwa kumsomesha, kwa sababu hawakuwa na uwezo wa kumlipia ada. Hapo akaangukia kukata tamaa kielimu na kurejea kwenye uzazi aliokwishaanza bila ya kupanga.

Kijana huyo anasimulia kwamba, safari ya kuwa mfanyabiashara akaianza mwaka 2023, baada ya waelimisha rika kutoka Mradi wa Kufikia Malengo katika Kudhibiti Maambukizi Mapya ya Virusi Vya Ukimwi- (Mradi wa wa EpiC) kutembelea nyumbani.

Hapo anasimulia akafunzwa ujasiriamali na baadae akashauriwa na wafadhili, ajiunge kwenye vikundi vyao viitwavyo 'Dreams', ili aweze kupata huduma nyingi zaidi.

"Baada ya mafunzo hayo, nilikubali kwenda kujiunga na kikundi kinachoitwa ' Overachiever Group' chenye wanachama 24, ambako aliweza kupata mafunzo zaidi.

Wakati wa mafunzo, Susana na wenzake anasema wakafundishwa elimu ya uchumi, kupanga bajeti, mawasiliano, jinsi ya kuandaa mpango biashara, kutafuta fursa mbalimbali za biashara.

Pia anataja kunufaika na elimu ya jinsia, uzazi wa mpango, ukatili wa kijinsia, kuweka akiba na kukopa, waliweza kupata huduma za afya, kupima afya, kufundishwa masuala ya uzazi wa mpango na magonjwa mengine ya ngono kama vile gono na kaswende.

Ni mafunzo anayotaja yalitolewa kupitia programu inayoitwa 'Determined, Resilient, Empowered AIDS-free, Mentored and Safe' au kwa kifupi chake, Dreams, wakafadhiliwa na taasisi ya USAID ya Marekani.

**BAADA YA MAFUNZO**

Hapo Susana anasimulia zaidi alichovuna, akitamka "baada ya kujiunga na kikundi cha Overachiever nashukuru Mungu nilikuwa mmoja wa mabinti waliochaguliwa kwenda kujifunza elimu ya ujasiriamali kwenye Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo Vidogo (SIDO)."

Anasema baada ya mafunzo kutoka SIDO, akachukua mkopo wa shilingi 100,000 kwenye kikundi chao, kisha akaanza kutengenezavyakula vya matunda na akauza sehemu mbalimbali mkoani Iringa na mpaka sasa mtaji wake umekua kufikia shilingi 500,000/-.

Susana anajivuna aliko kwa hatua ya maendeleo, akitamka: "Kwa kunifikia binti ambaye nilikuwa tegemezi, ambayo ingenipelekea kupata athari za maambukizi ya Ukimwi kutokana na vishawishi. Sasa hivi nimeanzisha biashara yangu, natengeneza 'jam' ya matunda aina mbalimbali na kuuza.

"Sasa hivi mimi siyo tegemezi, naweza kusaidia wazazi wangu, nimeweza kujenga nyumba ambayo hivi sasa kuna mpangaji na lengo kuu ni kujiongezea kipato zaidi,"anasema

Anaeleza, kupitia elimu ya uchumi ameweza kuwa na heshima katika matumizi ya fedha zake na kuweka akiba, akiamini baadae itamsaidia kukuza biashara zake.

Kwa mujibu wa Susana hadi sasa amefanikiwa kuweka akiba ya shilingi 472,000 kwenye kikundi chao kutokana na biashara yake, huku akitafuta fursa mbalimbali za biashara, akiidokezea Nipashe anauza kwenye maduka makubwa matatu ya Iringa.

Anasema, fedha anazopata kutokana na kuuza bidhaa zake, anapeleka kwenye kikundi chao, kwa sababu bado hajafungua akaunti benki, kwa kuwa bado hajapata kitambulisho cha NIDA.

Kingine kupitia elimu anayoipata, anasema kaweza kufundisha mabinti 30 jinsi ya kutengeneza 'jam 'ya matunda mbalimbali na kupanga bajeti waweze kuanzisha biashara zao, hata inawaepusha na vishawishi vinavyohatarisha maisha yao.

Susana anasema, pia kwa sasa yeye ni fundi bomba, ujuzi alipata baada ya kusoma kozi ya miezi sita ya taaluma hiyo katika chuo cha Donbosco Youth Training Centre mkoani Iringa, mwaka 2022 jana na mpaka sasa ameweza kujiajiri kujiongezea kipato.

Susana anasimulia alikotoka, baada ya kupata mimba na kushindwa kuendelea na masomo, aliangukia kuwa tegemezi wa kila kitu na akakata tamaa, akiamini majibu ya maendeleo yake yalikuwa ndani ya elimu shuleni.

"Wazazi waliniacha nyumbani, kwa sababu hawakuwa na uwezo wa kunilipia ada, lakini nashukuru Mungu baada ya kukutana na waelimisha rika kutoka mradi wa Epic, ambao walinisaidia kupata mafunzo ya aina mbalimbali hadi kufikia hapa," anatamka.

INAENDELEA UK.14

UCHUMI

# Dawa za kulevya zinavyotoboa mifuko maisha ya kila siku, wenye dhamana nao wakijipanga

## • Kombora kihistoria, dawa zilivyonaswa mtaani Dar na Iringa zaweka rekodi...

**Na Zanura Mollel**

UCHUMI ni nadharia inayozama katika namna ya kunufaika kwa kina kutoka rasilimali chache zilizoko. Hapo inajumuisha uzalishaji, usambazaji na matumizi ya rasilimali zilizoko.

Aina na tafsiri za uchumi zinaweza kugawanywa kulingana na muundo wa umiliki, mfumo uliopo kiuchumi na ngazi ya maendeleo husika.

Hapo kunaorodheswa uchumi wa soko huria, uchumi wa soko hodhi au wa kijamaa, uchumi wa mchanganyiko na uchumi wa kimataifa. Kimsingi, ni nadharia pana.

Uchumi unatajwa uko katika ngazi zote; mtu binafsi, kifamilia, hadi kitaifa na kimataifa, kulingana na azma, pia mazingira tajwa. Ila vyote hivyo vina uhusiano wa moja kwa moja na ndio maana leo, vita vya Ukraine na Russia, vinampa shida hadi raia mmoja mmoja.

Ndani ya nadharia hiyo uchumi, pia kuna nyendo zake, mfano katika mipango ya uchumi, uchumi wa fedha na kadhalika.

Kuna vitu vingi vinatajwa kuchangia kuporomoka uchumi katika taifa kama vile mizani ya biashara isiyolingana, au kushuka au kuporomoka kwa sekta muhimu kama za rasilimali na miundombinu.

Vilevile kunatajwa upungufu wa rasilimali au miundombinu duni, nao umo katika orodha ya vizuizi vya maendeleo ya uchumi. Uchumi na siasa, vina uhusiano wa moja kwa moja, msimamzi wa siasa, ndiye anaelekeza uchumi kufanya nini.

Hapo ndipo inapobainika usimamizi na maelekezo ya kisiasa, yanapokuwa na maelezo kimatendo ya ama uchumi kufanikiwa au la, huku nyuma yake zikiwamo, mathalan mabadiliko ya hali ya hewa, pia na majanga kama vile mafuriko, ukame, au matetemeko ya ardhi yanayoweza kuathiri uzalishaji na miundombinu.



Dawa za kulevya zilizochomwa shambani, wilayani Arumeru, mkoani Arusha. **PICHA: MTANDAO**.

**UCHUMI VS DAWA ZA KULEVYA.**

Vita dhidi ya dawa za kulevya vinaweza kuwa na athari kubwa kwa uchumi wa nchi. Kwa mfano, biashara haramu ya dawa za kulevya inatajwa kuchangia kwenye uchumi wa chini kwa kusababisha ufisadi, ukosefu wa usalama na kuharibu miundombinu ya kijamii.

Pia, kunatajwa juhudi za kupambana na dawa za kulevya zinazoweza kuwa sehemu muhimu ya sera za kiuchumi na kijamii.

Biashara ya dawa za kulevya inarejewa ni shughuli haramu inayosababisha madhara makubwa kwa jamii na uchumi wa nchi.

Nipashe imekuwa shuhuda kwamba, biashara hiyo mara nyingi inahusisha uhalifu wa kimataifa, ikiwa ni pamoja na biashara ya silaha na utumiaji nguvu, jambo linaloonekana kusababisha ongezeko la uhalifu na ukosefu wa usalama.

Biashara haramu ya dawa za kulevya, inatajwa kusababisha rushwa na kuharibu miundo ya kijamii kisiasa, hata kibiashara, ikishika nafasi ya juu duniani, sambamba na nyinginezo haramu kama za uuzaji binadamu, silaha na rushwa.

**ATHARI ZAKE**

Jumla zake zinatajwa kuchangia kuporomoka uzalishaji mali na uchumi wa taifa, kutokana na kundi kubwa la watumiaji kubweteka katika jinai.

Uchumi na maendeleo nao unaangukia kuathirika, kwa kuharibu sifa ya nchi na kuzuia uwekezaji kwenye taifa, linalokuwa na wimbi kubwa la mzunguko wa dawa za kulevya.

Sababu kuu kimsingi, ni hofu kwa mataifa mengine kuwekeza katika nchi hiyo, pamoja na hofu ya watalii kuingia nchini, jumla ya yote nchi inapoteza mapato na mtaji unaopaswa kuwekezwa.

Lingine ni matumizi ya dawa za kulevya, yanatajwa kusababisha matatizo ya kiafya kwa umma, kama vile magonjwa ya akili, kushuka kinga mwilini na kuangukia vifo, taifa likipoteza nguvukazi na ndio chanzo cha kushuka uzalishaji, pia umasikini wa umma.

**HALI YA UDHIBITI 2022**

Vita dhidi ya dawa za kulevya, kimsingi vinahusisha juhudi za serikali na jamii kudhibiti uzalishaji wake, usafirishaji na matumizi haramu ya dawa hizo. Pia, kuna atahri za kiuchumi za biashara haramu ya dawa za kulevya, zinazoangusha misingi ya uchumi na jamii.

Lengo la mamlaka hiyo kwa sasa linatajwa, ni kudhibiti upatikanaji wa dawa hizo, pia uhitaji wake, hata ngazi ya matumizi kudhibitiwa ili kudumisha ushirikiano wa kitaifa, kikanda na kimataifa katika mapambano yaliyoko.

Taarifa ya Hali ya Dawa za kulevya kwa mwaka 2022 iliyotolewa na Mamlaka (DCEA), inaonyesha kuwa uthibiti upatikanaji wa dawa za kulevya una sura zifuatazo:

Mwaka jana, tani 20.58 za bangi zilikamatwa, ikiwa na watuhumiwa 10,277; mirungi tani 15.23 ikiwa na watuhumiwa 1491; heroin kilo 254.71 yenye watu 409; cocaine kilo 1.73 na watuhumiwa 122. Pia, kuna methamphetamine gramu 97; na mescaline gramu 56.

**JITIHADA ZA MAMLAKA 2023**

Mara baada ya kuteuliwa kwa kamishna mpya Machi 16, mwaka jana, Aretas Lyimo, akaanzisha ofisi za kanda, kwa lengo la kurahisisha udhibiti wa viashiria vyote vya dawa za kulevya.

Ikirejewa taarifa aliyoiwasilisha kwa vyombo vya habari Dar es Salaam, Desemba 27 ,2023 Lyimo anasema operesheni iliyohusisha mkoa huo na Iringa, imefanikisha ukamataji mkubwa wa dawa za kulevya hata kuweka rekodi, toka kuanzishwa mamlaka hiyo.

Lyimo anataja dawa walizokamata ni aina ya heroin na methamphetamine jumla ikiwa na kilo 3,182 pamoja na watu saba wakiwemo wawili wenye asili ya Asia "Hawa tuliowakamata ni mtandao mkubwa wa usafirishaji, usambazaji wa dawa hizo, hatuwezi kuwataja majina bado taratibu za kimahakama zinaendelea".

Anafafanua kuwa heroini ni kilo 1001.7 na methamphetamine kilo 2,180.29 na zilikamatwa katika wilaya za Kinondoni, Kigamboni na Ubungo, mkoani Dar es Salaam na wilayani Iringa.

Anasema, dawa zilikuwa zimefungashwa kwenye bidhaa mbalimbali chupa za kahawa na majani ya chai, ikinuiwa kurahisisha usafirishaji wake, zisigundulike.

Kamishna Lyimo anafafanua kuwa kiasi cha dawa hizo zilizodhibitiwa, kama zingefanikiwa kuingia ndani ya jamii (mtaani), ingeathiri zaidi ya watu 76,368,00.

Anasimulia kuwa ukamataji huo, umeokoa nguvukazi iliyokua inaenda kuathrika kwa matumizi hayo tarajiwa ya dawa hizo.

**WAHUSIKA NA KINACHOENDELEA**

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alipozindua rasmi matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 jijini Dodoma, akatangza Tanzania ina jumla ya watu million 61,744,120, kwa mgawanyo; Tanzania Bara watu 59,851357 na Tanzania Zanzibar, wako 1,889,773

Maana yake ni kwamba, kiwango kilichodhibitiwa na Mamlaka ya Dawa a Kulevya, endapo dawa hizo zingefanikiwa kuingia katika mzunguko wa maisha ya Watanzania kingewaletea athari Watanzania 76,368,00. Inajenga maana, jumla ya Watanzania ambao wangebaki nje ya madhila hayo kiafya ni 54,107,320, ambao hawajafikiwa na dawa hizo.

Mtaalamu wa Uchumi na Biashara, Donati Ulomi,a nafaanua kwamba upo uhusiano mkubwa kati ya vita vya kiuchumi na matumizi ya dawa za kulevya.

Anaiambia Nipashe kuwa katika mataifa mengi yenye nguvu kiuchumi, yamekuwa yakidumaza taifa linaopambana kujikwamua kiuchumi kwa kuingiza na kusambaza dawa za kulevya.

Ulomi anataja dawa hizo zinadumaza nguvukazi na ninyie chake wanaowezersha biashara hizi wachache, ndio wanaopata fedha nyingi, kwa gharama ya kuiangamiza taifa.

Nchi inayotumia dawa la kulevya, anaitaja hunagukia umasikini, kutokana na kuwapo kundi kubwa tegemezi kwa taifa, serikali ikitenga fedha nyingi za kuwahudumia waraibu wa dawa za kulevya.

Pia, anasema kuna gharama ya kufanyika operesheni za kuthibiti wa mtandao huo wa uhalifu, kujenga vituo vya kutolea huduma kwa waraibu na kugharamia dawa kwa ajili ya matibabu.

Anashauri kuwa, ili kuwa na taifa lenye nguvu, mamlaka zinalizokasimishwa majukumu hayo inapaswa kuhakikisha inathibiti mianya ya Rushwa katika mtandao wa dawa za kulevya,kutoa elimu kwa makundi mbalimbali kuhusu athari za dawa hizo kiuchumi.

"Viongozi wanaopewa dhamana katika kuwaongoza watanzania wanapaswa kuwa mabalozi katika vita hii pamoja na kuchunguza vyanzo vya fedha na mzunguko wake nchini, ili kubaini kama ni mfumo halali wa kujipatia kipato," anatamka Mchumi Ulomi.

Kamishna Lyimo anasema, msimamo wa mamlaka yake ni kufanya operesheni endelevu katika maeneo mbalimbali nchini, akitoa rai watu wote wanaojihusisha na biashara na matumizi ya dawa za kulevya, waache mara moja, kwani kinyume chake sheria husika inachukua mkondo wake.



Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Aretas Lyimo, akiwa kazini. **PICHA: ZANURA MOLLEL.**

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Msikilizeni mtaalamu Profesa Janabi anakufaeni sana, acheni hizo bezo!






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com

HERI ya mwaka mpya Watanzania wenzangu! Waliotangulia mbele za haki kabla ya kuuona mwaka huu, bila shaka Muumba amewalaza mahali panapostahili, huku akiendelea kutufuatilia sisi na fujo zetu chini ya mbingu.

Kwa kweli Watanzania Mungu anatuangalia kinamna fulani na pengine hatujitambui. Nikikutazameni wenzangu nyie, huwa najiuliza na wakati mwingine kushangaa tupo duniani kufanya nini, hasa baadhi yetu tunaposhauriwa jambo na kulibeza sawia.

Hivi kweli ninyi mnaombeza Profesa Mohamned Janabi mna haki ya kufanya hivyo, kwa mtu anayejitolea kutoa elimu bure kwenu kuhusu kulakula yenu na ufakamiaji usio na tija wa kujaza matumbo, mpaka kulazimika kuwekwa maputo?

Hakika Profesa amepitia mengi na ameona mengi kwa wateja wake, ambao humfuata Muhimbili kupata huduma na kutokana na hilo, kwa wale anaoamini hawawezi kumfikia, huamua kutumia vyombo vya habari angalau kutoa bure ushauri nasaha.

Hebu fikiria, unaumwa unakwenda Muhimbili kumwona daktari mbobevu kama yeye, unadhani ada ya kumwona kwa wewe pangu pakavu tia mchuzi, itakuwa ni kiasi gani na akikubaini unaumwa kweli hayo matibabhu yake utayamudu! Thubutu!

Haya kaamua kujitolea akukinge na matatizo yanayoweza kukufikisha kwake, unambeza oh! mbona yeye yuko hivyo mbona yuko vile, kumbe yeye ana nia njema tu ya ubinadamu akusaidie, kutokana na aina ya maisha tunayoishi leo.

Watanzania kumbukeni, tulikotoka ni mbali na huko nyuma maisha hayakuwa haya ya kufakamia makemikali na kubwia mafuta tukishindana na magari kupitia vyakula tunavyokula leo. Yote hayo, Profesa Janabi ameyaona na ndiyo anayozungumzia, mabadiliko ya tabia na maisha.

Tutambue tu kwa,ba kuna mabadiliko makubwa sana ya kimaisha. Wangapi leo wanavaa saa? Wangapi wananunua redio? Wangapi leo wananunua kalenda? Ni nani ana simu ya mezani nyumbani kwake leo? Nani anapikia mafiga matatu mjini? Yote hayo ni mabadiliko na ndiyo dhana anayozungumzia Profesa kwa upande wa mlo na athari zake hasi.

Juzi nilikuwa na jirani yangu wa umri wangu, akanisimulia kuwa, kizazi chetu hiki kilichozaliwa kati ya miaka ya sitini mpaka angalau themanini hapo, ndicho cha mwisho kilichotembelea marafiki bila kulazimika kupiga simu bali kukutana chini ya mti au shambani na mazungumzo kumalizikia hapo.

Ni cha mwisho pia kuandikia barua wachumba au wapenzi na ujumbe ulifika bila matatizo, pia ndicho kizazi kilichocheza michezo mbalimbali pekupeku bila kujeruhiwa, cha mwisho pia kucheza kwenye mvua na kutoka hapo bila kupata homa.

Lakini, akasema ni kizazi cha mwisho kwenda msituni kucheza na kurudi nyumbani hata usiku mkubwa tena kikiwa salama kabisa, hata kiliporudi shuleni kikiwa na kazi za kufanya, kilifanya bila kusaidiwa na wazazi.

Ni kizazi cha mwisho pia kuendesha baiskeli masafa marefu, bila hata kofia ya chuma kichwani na bila kuumia, huku pia kikienda shuleni kwa miguu bila kulazimika kupelekwa kwa magari binafsi au ya umma (shule).

Akaniambia kizazi hiki ni cha mwisho kupata malaria na kumeza dawa za maumivu na kupona kwa siku mbili tu, pia kikipata uji na mahindi ya kuchemsha au kuchoma mchana na kufuatilia masomo darasani vizuri kabisa.

Jamaa yangu akasisitiza kuwa, kizazi hiki ni cha mwisho duniani kukaa wiki bila kufua sare za shule au kuoga na lisiharibike jambo na linafanya vizuri darasani, bila ya kutumia kikokotozi, kompyuta wala vitabu vya kiada.

Kizazi cha miaka hiyo ndicho cha mwisho kwa mujibu wa jamaa yangu huyu, kula pamoja kwenye sahani au bakuli moja la chakula, bila hata kunawa mikono na wasiugue. Wakati wa siku kuu kama Krismasi, kizazi hiki kilikula mkate wenye siagi, wali na nyama na kujisikia safi kabisa.

Ni kizazi ambacho mtu alibebab mzigo wa kilo 60 za mahindi kichwani na kupeleka kusagisha kwenye mashine, bila kulalamikia maumivu ya mishipa wala misuli na kiliogopa sana wazazi, hivyo hakikujibu kiliposemeshwa, kukaripiwa au kufokewa na mzazi huyo.

Kizazi hiki ndicho ambacho kikichapwa na mwalimu kilikuwa hakiendi kushitaki nyumbani kwa wazazi na kiliamini kuwa haki imetendeka. Pia ni kizazi cha mwisho kuchunga mifugo nyikani bila wasiwasi na kikiishi bila msongo wa mawazo au sonona.

Kwa kuwa alikuwa na mengi ya kuniambia, akahitimisha tu kuwa hiki ni kizazi cha mwisho kutembea pekupeku porini kwenye miiba ya kila aina bila kuathirika mbali na kuwa kizazi kilichojilawa mapema asubuhi na kufanya kazi za nyumbani na kisha kwenda shuleni umbali wa kilometa 20.

Kizazi cha kuanzia miaka ya tisini hadi leo kiko wapi? Kinaweza? Kinakula nini? Kinakunywa nini? Msikilizeni Profesa, yanayokufaeni chukueni yasiyokufaeni mwachieni, lakini si kumbeza! Mungu yu nasi na ni wetu sote!

UCHUMI

# Katibu Tawala Mkoa alivyozunguka kila tarafa kukagua miradi yake

## • Aibua 'madudu', akiagiza cha kufanya

**Na Ibrahim Yassin, SONGWE**

NI siku ambayo Katibu Tawala Happiness Seneda mkoani Songwe, akaamua kutembea mguu kwa mguu kukagua kazi za mkoa watendaji waliko.

Miongoni mwa miradi iliyotembelewa ni ya afya, elimu, miundombinu, maji, ujenzi wa vyoo na ukarabati wa majengo, ambao Katibu Tawala na timu yake, walipitia kwenye tarafa zote za mkoani humo, pamoja na kupokea kero za watumishi.

Ilikuwa na lengo kuitembelea miradi hiyo kutaka kujua jinsi fedha za serikali zinavyotumika, kukidaiwa bado ilikuwa na kasoro.

Katika miradi iliyoonekana ina kasoro, Katibu Tawala - Happines akatoa maelekezo akitaka marekebisho au maboresho yafanyike, miradi iendane na ramani maelekezo na thamani iliyotolewa na serikali.

Wiki ya kwanza ya ziara, ikaanzia wilayani Momba kwenye Halmashauri ya Tunduma na Momba, ambako pia kuna mpaka wa Tanzania na Zambia.

Huko akasema miradi mingi imejengwa kwa kufuata taratibu zilizowekwa, huku mapato ya ndani na nguvu za wananchi zikitumika.

Wiki iliyofuata, ilikaguliwa miradi wilayani Mbozi, ambako akakiri imejengwa vizuri kwa kufuata maelekezo, ingawa anakiri ipo baadhi iliyojengwa chini ya kiwango, baada ya vipimo vinavyotakiwa kwenda tofauti na ujenzi ulioko.



Katibu Tawala mkoani Songwe, Happines Seneda akizungumza na watumishi, baada ya kuhitimisha ziara yake ya kikazi ya kupitia miradi ya maendeleo mkoani huko. **PICHA: IBRAHIM YASSIN.**

Ilipokaguliwa miradi ya Mbozi, ziara ikasimama baada ya ujio wa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, aliyefanya ziara kiporo kukamilisha wilaya mbili za Ileje na Mbozi.

Baada ya hapo, Katibu Tawala akaendelea na ukamilishaji ziara aliyopanga wilayani Ileje na Songwe. Akiwa wilayani Ileje, pia akakagua miradi iliyojengwa vizuri, huku akitaja kuwapo iliyobainika kujengwa chini ya kiwango, ambako alitoa maelekezo.

Mapungufu makubwa wilayani Ileje. kukashuhudiwa kwenye Kitengo cha Ununuzi alikolaumu,huku akilalamika miradi mingi ya Elimu na Afya ilibainika kujengwa chini ya kiwango.

Hapo akamuagiza Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Nuru Kindamba kuchukua hatua kwa waliosababisha uzembe na upotofu wa fedha kwenye miradi ya zahanati na shule.

Ziara ikakamilika wilayani Songwe kwenye tarafa mbili, yaani Kwimba na Songwe, ambapo licha ya kuwapo miradi mikubwa na mizuri, changamoto iliyojitokeza kwenye Kituo cha Afya Kapalala, alikolalamika kukuta dawa zimetunzwa visivyo, hapo akatoa maelekezo maalum.

Siku iliyofuata ziara ikakamilika akisema amekuta tarafa ya Songwe, miradi mingi imejengwa vizuri na ipo yenye kasoro kiasi, ambako akatoa maelekezo pale palipoonekana upungufu.

Baada ya kumaliza ziara hizo, kukafanyika kikao cha majumuisho kwa kila wilaya ambako, akaelekeza na kuwakumbusha watendaji uwajibikaji, uzalendo, kuepuka wizi, kudhibiti mimba kwa wanafunzi huku walimu na wazazi wakibebeshwa jukumu la kutembea na wanafunzi.

Katika kikao wilayani Songwe, Katibu Tawala huyo akawaeleza watumishi kupiga vita vitendo vya ukatili, ulawiti, ubakaji ndoa za utotoni na mimba kwa wanafunzi, akisema sasa mkoa wa Songwe una asilimia 45 ya mimba na ukatili kitaifa.

Anaitaja kuwa aibu, hivyo akiwataka wenyeviti wa vijiji, watendaji vijiji na kata hadi viongozi ngazi ya wilaya wakiwamo wazee wa mila na viongozi wa dini kuungana kupinga vitendo hivyo.

Kuhusu wizi kwenye miradi, akasema kitengo cha ununuzi kifuatilie fedha zinazotolewa kununua vifaa vifaa vinafika sehemu husika, kwani kupelekwa kusikojulikana ni kashfa na hasa kitaifa, akiwahimiza wahandisi ngazi ya wilaya na mkoa kutembelea miradi na kutoa ushauri.

**UCHAKAVU MAJENGO SHULENI**

Mkuu wa Shule ya Msingi Udinde, Amani Kilagwa, kupitia kikao hicho akamuomba Katibu Tawala. amhamishe kwenye shule hiyo akidai kuwa majengo ni chakavu, yamejaa nyufa huku bati zikiwa zinavuja.

Akafafanua amedumu mahali hapo kwa zaidi ya miaka 10, lakini haikarabatiwi wala kujengwa, akielekeza ombi lake ahamishiwe Shule ya Msingi Oster Bay iliyopo kata ya Mkwajuni, ombi lililokubaliwa pasipo malipo.

Katibu Tawa akamjibu kwa kauli akasema aandike barua kwa Mkurugenzi wake (DED), ila hatalipwa fedha ya uhamisho na kuhusu uchakavu wa shule za zamani, akasema baada ya ujenzi wa shule mpya, serikali imeanza awamu ya kwanza kwa kutoa fedha kuzikarabati shule za zamani.

Pia, Katibu Tawala akawataka wazazi kuacha kuwatumikisha watoto kwenye maeneo ya machimbo ya dhahabu na kilimo, akikiri kuwa na ushuhuda binafsi.

Pia, akawataka watumishi kujiingiza katika uzalishaji mali kwa kulima kilimo cha mazao mbalimbali, kufuga na hata biashara, ila pasipo kuiba muda wa mwajiri.

Anasema, inakuwa na maana hata mtumishi akistaafu anakuwa na ahuweni kimaisha.

# Aliyenasa shule kwa mimba,yuko mlango wa pili kielimu na biashara

**INATOKA UK. 11**

**WAWEZESHAJI MRADI**

Kimsingi, ni mradi wa miaka mitano unaolenga makundi maalum yanayohitaji kipaumbele, wakiwamo wasichana wa rika balehe na kinamama vijana walio katika hatari ya kupata maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU).

Lengo hapo ni kuongeza upatikanaji huduma za kinga, upimaji na tiba, hivyo wanatoa mafunzo kuendeleza udhibiti wa maambukizi ya VVU, wakiimarisha usimamizi wa fedha za kutekeleza shughuli za VVU na kuzijengea uwezo asasi za kiraia, wakiziwezesha kupata ufadhili wa moja kwa moja.

Mkurugenzi wa Mradi wa Kufikia Malengo katika Kudhibiti Maambukizi Mapya ya Virusi vya Ukimwi (VVU), Bernard Ogwang, anasema Epic inatumika kwa miaka mitano, ikifadhiliwa na asasi ya USAID ya Marekani, ikilenga makundi maalum ikiwamo ya wasichana wa rika balehe na kinamama vijana kuanzia miaka 15 hadi25 walio hatarini kupata maambukizi ya VVU.

Ni mradi unaotekelezwa katika mikoa 18 na halmashauri za wilaya 58 Tanzania bara.

**MAFANIKIO YA MRADI**

Inatajwa kada za jamii hizo jumla yao, 220,123 wamefikiwa na mradi wa kuwakinga dhidi ya VVU na kati yao, wasichana husika 1294 waligunduliwa kuwa na VVU, 1207.

Pia, idadi ya asilimia 93 waliunganishwa kwenye vituo vya huduma ya tiba na matunzo (CTC) ili kufubaza VVU.

Hadi sasa kunatajwa jumla ya vikundi 126 vimeishasajiliwa katika mkoa wa Iringa, na vikundi viwili tayari vimeishapata mkopo wa serikali wenye thamani ya shilingi milioni sita kuendeleza biashara zao.

Pia jumla ya vitovu (Hubs) 16 za uwezeshaji mabinti kiuchumi wamevianzisha, vitovu viwili vipo katika wilaya ya Mufindi na hadi sasa jumla ya wasichana wa rika balehe na kina mama vijana 128 wamemaliza mafunzo hayo.

Anasema kati yao, 78 wamepata mafunzo ya ushonaji, 50 mafunzo ya komputa na 25 wamepewa elimu ya ufundi wilayani Mufindi na kupewa vifaa vya kuanzia mradi kama vile vifaa vya umeme, mapishi, fundi bomba, computa na ufugaji wa wanyama .

Hadi sasa jumla ya wasichana wa rika balehe na kina mama vijana 2247 wameweza kuanzisha biashara zao binafsi za kilimo, mboga mboga na matunda, uokaji wa bidhaa za aina mbalimbali, ufugaji wa mifugo, ufugaji kuku, maduka ya reja reja, ushonaji na usukaji wa bidhaa mbalimbali za vikapu na bidhaa nyingine.

Wapo pia 87, wameungwanishwa na Bima ya Afya ya Jamii (CHF), 11 wameunganishwa na kituo cha Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) mkoani Iringa.



# Shekhe awataka wanaoteuliwa na Rais kuacha unafiki

**Paul Mabeja na Peter Mkwavila** DODOMA

SHEKHE wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajabu, amewataka wateule wa Rais Samia Suluhu Hassan, kuutumia mwaka 2024 kujitathimini na kuacha kuwa wanafiki katika utekelezaji wa majukumu yao.

Pia, amewataka wateule hao kutimiza wajibu wao wa kuwatumikia wananchi wanyonge badala ya kuendelea kufanya mambo yenye maslahi yao binafsi.

Shekhe Rajabu, aliyasema hayo jana jijini hapa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mambo mbalimbali yaliyofanywa na serikali kwa mwaka 2023 na matarajio yake katika mwaka huu wa 2024.

Kiongozi huyo wa kiroho, alisema wateule wa Rais wanapaswa kuwa msaada katika kumsaidia kutimiza azma ya serikali ya kuwatumikia wananchi kwa kuboresha miradi ya elimu, afya, barabara pamoja na maji.

"Wateule wa Rais wawe msaada kwake katika kumsaidia kutimiza kile ambacho serikali imekiahidi kuwafanyia wananchi na wasiwe waongo ama wanafiki kwa wananchi wao. "Mnafiki ana alama tatu ya kwanza kila anapozungumza anasema uongo kila anachozungumza kwake siyo kweli alama ya pili ni kila anacho ahidi hatimizi anaahidi baada ya muda fulani kutakuwa na zahanati lakini ahadi hiyo haikamiliki hata mara moja na alama ya tatu akiaminika anafanya hiyana ameaminiwa na Rais lakini muda huo wote badala ya kuwatumikia wananchi anafanya mambo yenye maslahi yake binafsi" alisema.

Kadhalika alisema kutokana na hali hiyo wateule wa Rais pamoja na watumishi wengine wa umma wanapaswa kubadilika katika mwaka huu kwa kuacha kufanaya kazi kwa mazoea ili kusimamia kikamilifu miradi ya maendeleo.

Alisema siyo jambo la burasa wakati Rais anazunguka huku na kue kutafuta wadau mbalimbali ili kupata fedha za kuendesha miradi mbalimbili ya maendeleo wakati wateule wake wanashindwa kumsaidia kufikia azma yake.

"Rais Samia Suluhu Hassan, amejitahidi sana katika kipindi chake kujenga mahusiano mazuri ya kidiplomasia na mataifa mengine hali ambayo imesaidia kupata misaada na mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo lakini haitakuwa na maana kama wasaidizi wake watashindwa kumsaidia kusimamia maono yake" alisema Shekhe Rajabu

Akizunguzia kuhusu uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika mwaka huu, alisema Watanzania wanapaswa kuitumia demokrasia iliyopo nchini hivi sasa kupata viongozi waadilifu na wenye hofu ya Mungu.

"Bahati nzuri Rais tuliyenaye hivi sasa mama yetu Samia Suluhu Hassan ni muumini mkubwa wa masuala ya demokrasia hivyo lazima na hawa viongozi wa serikali za mitaa tutakaowachagua wawe wanademokrasia kwani kama mti ukinyooka hata kivuli chake kitanyooka pia"alisema Shekhe Rajabu.

Hata hivyo, aliwataka wazazi na walezi wenye watoto wanaostahili kuanza shule kuwapeleka kupata haki yao ya msingi wakati huu ambapo shule zinatarajiwa kufunguliwa kuanzia wiki lijalo.

Alisema: "Wazazi tuwapeleke shule watoto wetu hata wale wenye ulemavu hatupaswi kuwaficha tuwatoe ili wapate fursa hii ya kupata elimu kwani serikali imewekeza katika elimu pamoja na elimu kwa watu wenye mahitaji maalum".



Mkuu wa wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri akiwaonesha wasimamizi wa idara mbalimbali wa Jiji, plasta ya simenti iliyojengwa ambayo haiko imara iliyowekwa kwa ajili ya kujengea vigae kwenye vyumba vya madarasa yanayoendelea kujengwa Shule ya msingi Mayeto, iliyopo kata ya Hombolo Makulu Jijini Dodoma baada ya kufanya ziara yake jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Ajifungua watoto wanne, mumewe haifahamiki alipo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHADYA Mrisho (29) mkazi wa jijini Dodoma, amejifungua watoto wanne wa kike, huku mume wake haifahamiki alipo.

Akizungumza na waandishi wa habari katika wodi ya wazazi ya Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma baada ya kujifungua watoto hao Shadya alisema awali alilia alivyosikia ana watoto mapacha wanne kutokana na kuwaza kuwa atawahudumia vipi kwa sababu mume wake kwa sasa hafahamiki alipo.

Alisema akiwa hospitalini hapo alipata taarifa ya mume wake ambaye ni dereva wa magari makubwa kukimbia baada ya kupata ajali.

Shadya alisema baada ya kujifungua maziwa yalikuwa hayatoki kutokana na hofu aliyokuwa nayo.

Alisema hali ya kiuchumi kwake siyo nzuri lakini anaamini Mungu atamsaidia ili aweze kuwalea watoto hao ambao alijifungua mimba ikiwa na miezi saba kutokana na kuzidiwa uzito, hivyo madaktari wakalazimika kumfanyia upasuaji ili kuokoa maisha ya mama na watoto hao.

Alisema hivi sasa watoto wanaendelea vizuri chini ya uangalizi wa madaktari, kwamba muda wowote ataruhusiwa kwenda nyumbani.

Hata hivyo alisema alikuwa na mkakati wa kufunga kizazi lakini madaktari wamemshauri asifunge kutokana na umri wake wa miaka 29 aliokuwa nao. Alisema alitaka kufunga kizazi kwa sababu anaweza kushika mimba nyingine ambayo itampatia mapacha wengine kwa idadi kama hiyo.

"Nina watoto wawili tayari hivyo na hawa mapacha wanakuwa sita naogopa kujifungua tena nisijepata mapacha wengine wanne hali ya kiuchumi hainiruhusu kuwa idadi kubwa ya watoto" alisema.

Aidha, alisema anamshukuru Mungu yuko salama yeye na watoto wake huku akiwashauri kinamama wengine kuhudhuria kiliniki wakati wanapokuwa wajawazito ili wajue hali ya ujauzito wao pamoja na afya zao.

Kadhalika, aliwashukuru wauguzi wa hospital hiyo kwa huduma waliyompatia muda wote aliokuwepo hapo hadi kujingua salama yeye pamoja na watoto wake.

Alisema: "Naishukuru pia serikali kutokana na kuweka bajeti kubwa kwa Wizara ya Afya inayosaidia wananchi kupata huduma bora kutoka kwenye hospitali mbalimbali hapa nchini" alisema.

# Wakazi Bahi Sokoni waiomba serikali ujenzi daraja

**Na Paul Mabeja,** BAHI

WAKAZI wa Kijiji cha Bahi Sokoni wilayani Bahi mkoani Dodoma, wameiomba serikali kutengeneza miundombinu ya Daraja la Mto Bubu ambalo limebomoka kutokana na mvua zinazonyesha na kusababisha kukatika kwa mawasiliano na vijiji jirani.

Ombi hilo lilitolewa jana na wakazi wa kijiji hicho walipokuwa wakizungumza na waandishi wa habari kuhusu kuharibika kwa Daraja hilo.

Mmoja wa wakazi hao, Omary Abdalla, alisema mvua zinazoendelea kunyesha zimesababisha kubomoka kwa daraja hilo ambalo wanalitegemea kuvuka kwenda katika shughuli mbalimbali za uzalishaji mali.

"Daraja hili tunalitegemea kuvuka wakati wa kwenda kwenye shughuli mbalimbali ikiwemo kilimo wakati huu ambapo mvua zinaendelea kunyesha katika wilaya yetu" alisema.

Aidha alisema hivi sasa kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha maji yamesomba sehemu ya miundombinu ya daraja hilo hali ambayo inasababisha wakulima kushindwa kwenda kwenye shughuli zao za kilimo.

Alisema wanaiomba serikali kulifanyia kazi suala hilo ili wapate daraja lenye viwango ambalo litatumika muda wote bila kujali wakati wa masika au kiangazi.

"Kama mnavyoona hivi sasa daraja limejaa maji halipitiki ni hatari kwa maisha yetu tunaomba serikali itusaidie kujenga miundombinu ya daraja hili ili tulitumie kwenda kwenya shughuli zetu za uzalishaji mali"alisema

Hata hivyo, alisema kubomoka kwa daraja hilo kumesababisha uhabifu wa skimu za umwagiliaji wa zao la mpunga ambalo linategemewa kama zao la biashara wilaya hapa.

Naye, Katibu wa skimu ya umwagiliaji ya Nguvu mali wilayani hapa Mussa Abdalla, alisema wanaiomba serikali kutengeneza miundombinu ya daraja hilo ambalo limebomoka kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha ili kuokoa mazao yao.

Alisema mvua zinazoendelea kunyesha maji yanapita juu ya daraja hali inatishia uhai wa watu, uharibifu wa miundombinu ya skimu za mpunga na baadhi ya wakulima kushindwa kuendelea na kilimo kwa hofu ya kusombwa na maji.

Meneja wa Wilaya ya Bahi wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mjini (TARURA), John Chalula, alisema daraja hilo linatumika na wakulima wa mpunga.

Alisema daraja hilo limekuwa na changamoto hasa wakati wa kilimo kutokana na kuwa ni daraja la chini hivyo mvua ikinyesha maji yafunika na wakati mwingine inafika hadi mwezi.

Alisema: "Changamoto tuliyonayo ni bajeti tumekuwa tukiliombea fedha daraja hili kupitia miradi ya maendeleo lakini hatupati na linahitaji fedha nyingi takribani bilioni tatu".





# Ujenzi wa shule wasaidia wanafunzi kutembea umbali mrefu

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANANCHI wa Kata ya Makowo Halmashauri ya Mji Njombe Mkoa wa Njombe, wameishukuru serikali kwa kuwajengea shule mpya ya sekondari katika kata hiyo.

Wamesema ujenzi wa shule hiyo iitwayo Matola itawapunguzia wanafunzi adha ya kutembea umbali mrefu.

Waliyasema hayo katika mkutano wa hadhara ambao uliokuwa na lengo la kutatua changamoto mbalimbali za wananchi na kuangalia utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika kata hiyo.

Walisema miundombinu mizuri ya shule haikuwahi kuletwa hivyo ni faraja kwa wakazi hao katika kuinua elimu katika kata hiyo na kuongeza mwamko wa watoto kwenda shule.

"Nimekuwa nikiwapeleka watoto shule hadi Kata ya Matola ambapo ni mbali sana. Lakini kwa sasa shule mpya ambayo tumejengewa hapa naimani itatuvusha kwenda hatua nyingine ya mafanikio, nitakuwa naenda kuangalia maendeleo ya mtoto wangu kama anaendelea vizuri, kweli mnyonge mnyongeni haki yake mpeni Rais Samia Suluhu Hasaan ametusaidia sana wana Makowo," alisema Saraphina Nziku.

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Njombe, Julius Peter aliwaomba wanachi wa Kata ya Makowo kukiamini chama hicho ambacho kinatekeleza ilani.

Alisema chama hicho kitaendelea kufanya maendeleo makubwa hasa kuwasogezea wananchi mahitaji mhimu ya umeme kama shule, huduma za afya na barabara.

Alisema: "Ni muda sasa wananchi kukiamini chama cha mapinduzi kinachoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan ndiye anayefanya haya yote mnayoyaona, shule mpya iliyopo Makowo yenye thamani ya Sh.milioni 583

"Fedha hizi hazijaja kwa muujiza ni kujituma kwa viongozi wetu mpaka mnaona hizi fedha ni muda sasa wa kumwamini na kuendelea kuiunga mkono CCM," alisema Kachinga.

Naye Kaimu Ofisa Elimu Sekondari, Rehema Nswila aliwaomba wananchi wa kata hiyo kuwapeleka watoto shule kwani tayari walimu wameshawasili katika shule hiyo tayari kwa kuanza masomo Januari 2024.

# Wanging'ombe waonywa tabia kutowapeleka watoto shule

**Na Elizabeth John,** WANGING'OMBE

WAZAZI na walezi wilayani Wanging'ombe katika Mkoa wa Njombe, wametakiwa kuhakikisha wanafunzi 4,823 ambao wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu, wanaripoti kwa wakati badala ya kuwatumikisha kwenye shughuli za uzalishaji.

Wanafunzi hao wamechaguliwa kuanza kidato cha kwanza katika shule 23 za sekondari zilizopo wilayani hapa ambapo wavulana ni 2,269 na wasichana 2,554.

Wito huo ulitolewa na Kaimu Ofisa Elimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, Samson Machibya wakati akizungumza na Nipashe.

Aliwataka wazazi kuwaandalia watoto mahitaji ya msingi ikiwemo madaftari.

"Serikali imeshafanya kwa upande wake kuandaa miundombinu na kuwahatarisha wanafunzi ambao wanatakiwa waingie darasa la kwanza, upande wa wazazi nawahimiza wafanye maandalizi wawaandae watoto vizuri kwa maana ya kuwaandalia mahitaji muhimu kwa maana ya madaftari na vifaa vyengine vinavyohitajika," alisema Mashibya.

Mashibya alisema kumekuwa na uzoefu wa wanafunzi kuchelewa kuripoti kidato cha kwanza hali ambayo inasababishwa na wazazi kutofanya maandalizi mapema.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, Onesmo Lyandala alisema miaka ya nyumba kulikuwa na changamoto ya watoto kutoripoti shule na kujishughulisha na shughuli za kiuchumi lakini kwa sasa wote wanatambua umuhimu wa elimu.

"Sina shaka na miaka hii lakini miaka ya nyuma kulikuwa na changamoto ya kuweza kuripoti kwa wakati kutokana kuwa na maeneo yetu yanauchumi mkubwa sana kwa hiyo watoto walikuwa wakishawishika na kupata fedha hasa kipindi hiki cha likizo," alisema Lyandala.

Hata hivyo Diwani wa Kata ya Itulahumba, Thobias Mkane na Diwani wa Kata ya Wanging'ombe, Geofrey Nyagawa waliwataka wazazi kuhakikisha watoto wao wanaripoti shuleni na kueleza kuwa kwa wale watakaokadi wachakuliwa hatua za kisheria.

"Wazazi wanatakiwa wajue ni wajibu wao inapofika tarehe nane mwaka huu mapema waweze kuwapeleka watoto shule na hivi ninavyozungumza waanze kuandaa vile vitu ambavyo vinawahusu wao kwa maana ya madaftari na vitu vingine vidogo vidogo ambavyo vinaweza vikamfanya mtoto inapofika tarehe nane aweze kufika shuleni," alisema Mkane.

Mkane alitoa rai kwa wazazi wa Kata ya Itulahumba kwamba hatarajii kutumia nguvu katika kuwahimiza wazazi kupeleka watoto shule na badala yake kila mmoja atimize wajibu wake.



Mmoja wa vijana waendesha bodaboda wa Jiji la Mbeya akisafirisha matenga ya nyanya kwa kutumia pikipiki katika eneo la Nzovwe kwenye Barabara Kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM) huku akiwa amevaa kandambili na hajavaa kofia ngumu jambo ambalo ni hatari kwa usalama wake. **PICHA NA NEBART MSOKWA**

# Babalishe, mamalishe wapewa msaada mitungi ya gesi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

Mbunge wa Njombe Mjini mkoa wa Njombe, Deo Mwanyika ametoa msaada wa mitungi ya gesi kwa baba lishe na mama lishe wanaofanya kazi kwenye Kituo cha Mabasi cha Njombe Mjini kilichopo kwenye kata ya Mji Mwema ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira.

Ugawaji wa mitungi hiyo ulifanyika mjini hapa, Mwanyika alisema ametoa mitungi kwa makundi hayo akiwa na lengo la kuendelea kuiunga mkono serikali katika jitihada za kuhamasisha wananchi kutumia nishati safi.

Mwanyika alisema matumizi ya gesi yatawasaidia kuondokana na matumizi ya kuni na mkaa ambao umekuwa ukisababisha madhara ya kiafya kwa watumiaji.

Hata hivyo Mwanyika alisema anatamani kuona baba lishe na mama lishe wanakuwa chachu ya utunzaji wa mazingira kwa kuingia kwenye matumizi ya gesi kuliko kuendelea kuharibu mazingira kwa kutumia kuni pamoja na mkaa.

"Nia yetu ni kutaka muendelee kutumia gesi wakati wa kuandaa vyakula na matumizi mengine, tuache kukata kuni na kuchoma mkaa hasa maeneo ya mjini na zoezi hili litakuwa ni endelevu kwenye maeneo mengine," alisema Mwanyika.

Mwenyekiti wa mama lishe na baba lishe wa kituo hicho, Happy Msango kwa niaba ya wajasiriamali hao alitoa shukrani kwa msaada huo huku pia wakiomba kurekebishiwa changamoto ya miundombinu ya jengo lao linalotumiwa wakati wa kuandaa chakula ikiwemo urekebishwaji wa sakafu ambapo Mwanyika alitoa ahadi ya kushirikiana na halmashauri ili kufanya marekebisho hayo.

Msango alisema: "Mh. mbunge tunashukuru sana kwa msaada huu kwa sababu unakwenda kuokoa afya zetu, lakini kuna changamoto hapa ya sakafu tunaomba turekebishiwe".



## Serikali kuipiga 'msasa' Barabara ya Kiembesamaki-Mtoni

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema serikali inaratajia kuijenga Barabara ya Kiembesamaki hadi Mtoni ili iweze kutumika kwa shughuli za usafiri na usafirishaji.

Aliyasema hayo jana Uwanja wa Garagara Mtoni Kidatu katika Wilaya ya Magharib 'A' Unguja wakati akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa barabara hiyo (Km 8.5) inayojengwa na Kampuni ya CCECC kutoka nchini China.

Alisema kwamba barabara hiyo inazaidi ya miaka 40 iliyojengwa kwa awamu tatu tofauti na awali serikali ilikuwa ikifanyia matengenezo madogo ya kila mara ikiwa ni pamoja na uzibaji wa mashimo.

Aidha alisema kwamba ujenzi wa barabara hiyo pia utakwenda sambamba na ujenzi wa madaraja mawili (flyover), katika eneo la Mwanakwerekwe na Amani ili kupungunza msongamano na foleni katika maeneo hayo.

Alisema mbali na madaraja hayo yatakapokamilika kuondoa changamoto ya msongamano wa magari katika maeneo hayo, pia itasaidia kuleta mwonekano mzuri wa Jiji la Zanzibar.

Pia aliwataka wananchi kuendelea kuwa na subira na uvumilivu katika kipindi hiki ambacho ujenzi unaendelea kutokana na kuwepo changamoto ya vumbi na baadhi ya barabara kufungwa na kusababisha usumbufu kwa wananchi wakati wa shughuli zao.

Alisema mafanikio hayo yasengepatikana bila ya kuwepo uzalendo wa wananchi kuendelea kulipa kodi ili kuunga mkono jitahada za serikali.

Akizungunzia suala la fidia kwa wananchi walioathirika kutokana ujenzi huo aliwataka wananchi kuendelea kuwa na subira na kwamba serikali inafanya jitihada kuhakikisha kila mmoja analipwa.

Othman aliitaka jamii kukumbushana juu ya haja na umuhimu wa kuwepo malezi bora kwa watoto na vijana ili kuwalinda na majanga, tabia na mazingira hatarishi yakiwemo ya ukatili, udhalilishaji na matumizi ya dawa za kulevya.

Alisema kwamba kufanya hivyo ni kusaidia taifa kupata nguvu kazi imara na makini kutokana na kuwepo kizazi bora kinachoweza kutoa mchango mkubwa katika kupambana na jitihada za kutafuta maendeleo ya taifa.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohammed, alisema ujenzi wa madaraja ya juu yanatarajiwa kuwa madhubuti zenye uwezo wa kuhimili uzito mkubwa wakati utakapokamilika.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Khadija Khamis Rajab, alisema ujenzi wa barabara hiyo pamoja na madaraja yake tayari Sh. bilioni 8.5 zimeshatumika kumlipa mzabuni kutokana na kazi hiyo inayoendelea.

# Karume ataja siri ya wawekezaji kukimbilia Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS Mstaafu wa Zanzibar, Abeid Amani Karume amesema Zanzibar inaendelea kupata wawekezaji wengi kwenye miradi kunakochangiwa na uwepo wa amani na utulivu.

Aliyasema hayo jana wakati akizindua mradi wa hoteli ya kitalii yenye hadhi ya nyota tano iitwayo 'Y' corner iliyopo Urowe Pongwe Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema wawekezaji wengi hivi sasa wanahamu na shauku ya kufika Zanzibar kuwekeza katika miradi yao ya maendeleo ikiwemo hoteli za kifahari kwa vile Zanzibar imeonekana kuwa na haiba nzuri na amani iliyopo.

Alisema katika kuhakikisha kuwa uchumi wa Zanzibar unakuwa na kuzidi kuwavutia wawekezaji wananchi wanatakiwa kufahamu kuwa walimu wazuri katika utunzaji wa amani pia na mazingira yaliyopo.

Alisema awali hakukua na muwekezaji anayeweza kuwekeza katika sehemu iliyojaa migogoro na ambayo haina haiba nzuri ya kuvutia katika mazingira lakini kwa sasa mambo yamebadilika.

Karume alisema serikali kupitia taasisi ya uwekezaji imekuwa mstari wa mbele katika kuitangaza Zanzibar katika nyanja ya uwekezaji.

Aidha alisema Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) hivi sasa imekuwa na ubunifu mkubwa wa kutumia nyenzo za kidigitali katika ufanyaji wa kazi na hivyo ndiyo chanzo cha kuondosha ukiritimba wa kufanya kazi.

Alisema wawekezaji wanaokuja kuwekeza Zanzibar lazima wafahamu kuwa nafasi za ajira wanatoa kwa wazawa ili kuwanufaisha.

Pia aliitaka ZIPAishirikiane na wawekezaji katika kutoa elimu juu ya utunzaji wa mazingia.

Naye waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Uwekezaji, Mudri Ramadhan Soraga, alisema mradi huo wa muekezaji umekuwa na utofauti kidogo na wawekezaji wengine kwa sababu mwekezaji huo amekuwa mtunzaji wa kuhifadhi mazingira kwa kupanda miti ili kuwa na haiba nzuri katika hoteli hiyo.

Alisema mwekezaji wa hoteli hiyo anashirikiana vizuri na wanyeji wa maeneo hayo na tayari ameshaajiri vijana 150 katika hoteli hiyo ili kujikwamua na hali zao za maisha.

Alisema hivi sasa ZIPA imeshaandaa sheria kwa ajili ya uwekezaji na hivi karibuni sheria hiyo itatiwa saini na kuanza kutumika.

Mkurugenzi wa ZIPA, Sharif Ali Sharif alisema katika kipindi hiki cha miaka mitatu zaidi ya vijana 17,000 wameshapata ajira kupitia uwekezaji visiwani humo. Alisema katika kipindi hicho miradi 296 imeshawekezwa huku miradi 112 ikiwa ni miradi ya utalii hiyo ni moja ya mafanikio kwa upande wa serikali na serikali imefanikiwa kuingiza Dola za Marekani bilioni 4.5.

Sharif alisema bado ZIPA inamuamko mkubwa wakuwashawishi wawekezaji wengi kuwekeza Zanzibar kwa maslahi ya Wazanzibari na Watanzania. Meneja Mwendishaji wa hoteli hiyo, Emmanueli Johnson, alisema mradi wa hoteli hiyo itakapokamilika itakuwa na vyumba 40 vyenye hadhi ya kimataifa na wamejipanga kuhakikisha kuwa mambo yanaenda vizuri.

Alisema uwekezaji wao umelenga zaidi katika utunzaji wa mazingia katika maeneo hayo kwa sababu wanafahamu kuwa mazingira yakiharibika ni maafa katika taifa lolote.

Alisema malengo mengine ya uwekezaji wao ni kuwasaidia wavuvi wa maeneo hayo kuwatunzia samaki wao katika mitambo ya barafu.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma (wa pili kulia), akikata utepe kama ishara ya kufungua tawi la Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) Nungwi, wilaya ya Kaskazini A, ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yajivunia huduma bora miaka 60 ya mapinduzi

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, amesema serikali imeimarisha huduma za afya, elimu, maji safi na salama, mawasiliano na uchukuzi ili kuendana na dhamira ya mapinduzi ya mwaka 1964 ya kuwaletea wananchi maendeleo.

Alisema hayo yote yanaenda sambamba na uimarishwaji wa dhana ya uchumi wa buluu ambayo ndiyo ajenda ya kitaifa serikalini. Akifungua kongamano la kuadhimisha miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar Hemed, alisema malengo ya mapinduzi yalilenga kuondoa ukoloni na kuimarisha uchumi na kuwaletea maendeleo wananchi.

"Serikali inaendelea kuimarisha miundombinu mbalimbali ambapo kwa upande wa afya imefanikiwa kujenga hospitali 10 za wilaya na hospital moja ya mkoa iliyopo Lumumba pamoja na kujenga na kukarabati vituo vya afya na ujenzi wa nyumba za madaktari kwa Unguja na Pemba" alisema.

Aidha alisema serikali imefanikiwa kujenga shule 64 kati ya hizo shule 34 ni za ghorofa.

Hemed alisema serikali imeimarisha mazingira bora kwa wafanyabiashara wakubwa na wadogo kwa kujenga masoko makubwa na ya kisasa yakiwemo Soko la Mwanakwerekwe, Jumbi na Chuini kwa lengo la kuwawekea wafanya biashra mazingira mazuri.

Aidha alisema serikali itahakikisha inayafanyia kazi mapendekezo na maazimio yatakayotolewa katika kongamano hilo ambayo yatasaidia katika kufikia maendeleo ya nchi pamoja na kuwataka wananchi kuendelea kuwa wasikivu na watulivu kwa kuipa ushirikiano serikali.

Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita, alisema malengo ya kufanyika kwa mapinduzi ni kuimairisha uchumi wa Wazanzibari ambao wengi wao ni wakwezi na wakulima.

Pia kuimarisha amani na uzalendo kwa wananchi ambapo maono na falsafa zao zinaendelea kudumu na kuenziwa kwa maslahi ya taifa.

Tabia alisema kufanyika kwa kongamano hilo kunatoa fursa kwa wale wote waliozaliwa baada ya mapinduzi kufahamu dhana nzima ya kufanyika kwa mapinduzi ili kujua umuhimu wake na namna ya kuyalinda na kuyaenzi Mapinduzi ya Zanzibar.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**HURA RAMADHANI CHUU** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne Index No. **Haikumbuki** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia KOLO SECONDARY SCHOOL mwaka 2020, Pamoja na cheti cha kuhitimu darasa la saba. Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/270/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SAUKO PILULA TIMOTH** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 407 DTV – SUBARU IMPREZA y**enye Chassis namba **GH2049305, Engine namba EL15E415198.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/KIN/56956/2023.**

## KUPOTELEWA NA KADI ZA PIKIPIKI

**Ndugu ZAHARANI SIRAJI TWAIBU** anatangaza kupotelewa na kadi za pikipiki zenye namba za usajili **MC166 ABJ na MC 663 AAC.** Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **PHQ/KAG/BUK/3/2024.** Kwa yeyote atakayeziona atoe taarifa polisi au apige simu namba **0789987497.**

District Land and Housing Tribunal Regulation GN No. 174/2003
Form No. 2B

**BARAZA LA ARDI NA NYUMBA LA WILAYA YA KINONDONI**

**MAHALI: M/NYAMALA**

**MAOMBI NA. 284 MWAKA 2022**

**UPENDO RAYMOND MARWA...............MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**MBWANA .P. ISSA..........MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA; MBWANA P. ISSA**

Mdai/wadai/amefungua/wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba dhidi yako/yenu. Shauri hilo limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 17 Mwezi 01 Mwaka 2024 saa 03:00 asubuhi mbele ya **Mh. J.M. SILLAS** Mwenyekiti wa Baraza.

Unatakiwa/mnatakiwa ufike/mfike wewe mwenyewe/ninyi wenyewe au wakili wako/wenu, mwakilishi wako/wenu pasipo kukosa na ulete/mlete utetezi wako/wenu ndani ya siku ishirini na moja (21) toka tarehe ya kupokea kuitwa shaurini.

**AMRI** hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 21 Mwezi 11 Mwaka 2023.

MWENYEKITI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na. 02/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU IDDI MOHAMED wa Chang'ombe**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA RAMADHAN IDDI MOHAMED**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 18 Mwezi 01 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 03 Mwezi 01 Mwaka 2024.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**S & Y WOOD PRODUCTS COMPANY LIMITED** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 246 DFS** aina ya **FOTON,** Chassis No. **LVBS6PEB9FL004696,** Engine No. **1115C001068.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/405/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SAID MOHAMED HURUVI** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye jina **MAYUNGA ATANAS MASHOKELO** namba za usajili **MC 736 DLK** aina ya BOXER, Chassis No. **MD2B15BX6NWB97593.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/MAN/KIT/32/2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**

**MAHALI DODOMA**

**MAOMBI MADOGO NA. 340 YA MWAKA 2024**

**BAINA YA**
**DANIEL CHISANZA MHIMILI.......................................MDAI**

**DHIDI YA**

**SKOLASTIKA GIBORE..................................MDAIWA**

**KWA: SKOLASTIKA GIBORE**
**POPOTE ULIPO.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo untakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 31.01.2024asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
**ANGALIZO:** - Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea Hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 03 ya Mwezi February, 2022

MWENYEKITI
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0745 700 710.*

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701
AU
TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Trump apinga kuondolewa kwenye karatasi ya kura

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS wa zamani wa Marekani, Donald Trump, ameiomba Mahakama ya Juu ya Marekani kubatilisha uamuzi wa kuzuia ugombea wake katika jimbo la Colorado, na kuanzisha mzozo wa hali ya juu kuhusu iwapo kifungu cha katiba kinachokataza wale wanaojihusisha na uasi kitamaliza medani yake ya kisiasa.

Trump alikata rufaa dhidi ya uamuzi uliongwa mkono na majaji wanne dhidi ya watatu mwezi Desemba, 2023 na Mahakama ya Juu ya Colorado ambayo ilikuwa mara ya kwanza katika historia kutumia kifungu cha tatu cha marekebisho ya 14 ya katiba ambacho kilitumiwa kumzuia mgombea urais kuwepo kwenye karatasi ya kura.

Ilibainishwa kuwa Mahakama iliona kwamba ushiriki wa Trump katika tukio la Januari 6, 2021, katika bunge la Marekani lilimnyima haki chini ya kifungu hicho.

Aidha, ilielezwa kuwa sheria hiyo imetumika kwa kiasi kidogo katika historia ya Marekani, na hivyo Mahakama ya Juu nchini humo haina uamuzi wa mfano juu ya shauri hilo. **VOA**

# AU na Marekani zataka Somalia iheshimiwe

**MOGADISHU,** SOMALIA

UMOJA wa Afrika na Marekani wametoa wito wa kutaka taifa la Somalia kuheshimiwa katika mamlaka yake, tamko ambalo limekuja baada ya kuwekwa kwa makubaliano ya mkataba wa bandari kati ya Ethiopia na Somaliland.

Ilielezwa kuwa mkataba huo ulioingiwa siku chache zilizopita umesababisha mvutano wa kidiplomasia, huku Somalia ikilaani na kuita ni kitendo cha uchokozi na ukiukaji wa uhuru wake na kuapa kuupinga kwa njia yoyote ya kisheria.

Somaliland ilijitenga kutoka Somalia tangu mwaka 1991 lakini haitambuliki kimataifa kama taifa huru.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje wa Marekani, Matthew Miller alisema kuwa Marekani inatambua uhuru na uadilifu wa eneo la Jamhuri ya Shirikisho la Somalia ndani ya mipaka yake.

Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika, Moussa Faki pia alihimiza kuheshimiwa kwa umoja, uadilifu wa eneo na mamlaka ya Somalia na Ethiopia.

Marekani na Umoja wa Afrika pia zimetaka pande zinazohusika kuendeleza mazungumzo ya kidiplomasia ili kutatua mzozo huo kwa amani, licha ya kuwepo kwa wasiwasi kwamba huenda makubaliano hayo yanaweza kuzidisha mvutano katika eneo hilo. **BBC**

# Kauli ya Rais Ruto yaendelea kukosolewa

**NAIROBI,** KENYA

RAIS William Ruto ameendelea kukosolewa kwa kauli yake kuwa serikali yake haitaheshimu maamuzi ya Mahakama, yatakayopinga miradi ya serikali yake, akiwashutumu baadhi ya majaji kuwa mafisadi na wasiojali maslahi ya umma.

Siku chache zilizopita, Rais Ruto alisema kuwa baadhi ya majaji ambao hakuwataja wanashirikiana na wanasiasa wa upinzani pamoja na watu wenye nia ya kuzuia kuendelea kwa miradi ya serikali.

Jaji mkuu kwenye taifa hilo la Afrika Mashariki, Martha Koome, wakati akijibu kauli hiyo ya kiongozi wa nchi, alieleza kuwa kukiuka maamuzi ya mahakama ni kinyume cha sheria kwa watumishi wa umma.

Aidha Jaji Mkuu pia aliwataka Majaji wa Mahakama kuendelea na kazi yao kwa mujibu wa sheria za nchi bila ya uoga na upendeleo.

Kiongozi wa upinzani Raila Odinga, alisema uamuzi wa Ruto ni hatari kwa demokrasia ya nchi hiyo.

"Vita hivi sio tu kuhusu Mahakama, bali ni mpango wa Ruto kuipotosha Kenya baada ya kuliteka bunge, sasa anataka kuiteka Mahakama." alisema Odinga.

Chama cha Mawakili nchini humo, nacho kimetangaza kuwa kitaandaa maandamano ya nchi nzima, kupinga kauli ya Ruto wanayosema ni kuishambulia Mahakama na Majaji.

Rais Ruto kupitia taarifa iliyotolewa na msemaji wa serikali Hussein Mohammed juzi, alikiri kuendelea na vita dhidi ya kile alichokitaja kama Mahakama kutoonekana kutochukuliwa hatua.

Ruto aliyeingia madarakani mwezi Septemba 2022, pia ametuhumiwa kwa kuwaongezea raia wa Kenya ushuru kwenye bidhaa mbalimbali haswa wakati huu wanapokabiliwa na ugumu wa maisha.

**RFI**



Kikosi cha zimamoto kikiwa katika juhudi za kunusuru watu katika jengo lililoporomoka mjini Wajima nchini Japan baada ya kukumbwa na tetemeko la ardhi siku chache zilizopita, hali inayotajwa kusababisha vifo 73 hadi jana. **PICHA: MTANDAO.**

# Kesi ya Afrika Kusini dhidi ya Israel yaiva

**PRETORIA,** AFRIKA KUSINI

MAHAKAMA ya juu ya Umoja wa Mataifa ya Haki (ICJ) itasikiliza shauri la Afrika Kusini, na Israel, wiki ijayo baada ya Pretoria kufungua kesi kwa kile ilichokiita mauaji ya kimbari ya Israel huko Ukanda wa Gaza.

Katika kesi ambayo Afrika Kusini imeifungua inaitaka Mahakama ya Kimataifa ya Haki kuamuru kwa haraka Israel kusitisha operesheni zake za kijeshi huko ukanda wa Gaza.

Aidha, Marekani iliikosoa Afrika Kusini, kwa kuwasilisha kesi ya mauaji ya kimbari, na kupinga shutuma dhidi ya Israel kuhusu vita vyake huko Gaza.

Msemaji wa Baraza la Usalama wa taifa la Marekani, John Kirby, alisema uwasilishwaji huo hauna maana, tija na msingi wowote.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani, Matthew Miller alisema kwamba kutokana na tathmini ya Marekani, hawajaona vitendo vinavyojumuisha mauaji ya kimbari kwa wakati huu.

"Mauaji ya kimbari hakika ni uhalifu wa kutisha. Haya ni madai ambayo hayatakiwi kutolewa kirahisi rahisi tu," alisema.

Afrika Kusini, ambayo mara kwa mara imeikosoa Israel kwa namna inavyowachukulia Wapalestina, imeyafananisha matukio yanayofanywa na Israel na historia ya utawala wa kibaguzi nchini humo, na kuishutumu kwa kufanya visa hivyo kwa malengo maalumu ya kuwaangamiza Wapalestina walioko huko Gaza.

Afrika Kusini inataka kutolewa amri itakayoilazimisha Israel kusitisha operesheni zake za kijeshi katika Ukanda wa Gaza.

Katika hatua nyingine, Ujerumani na Ufaransa zimekosoa matamshi yaliyotolewa na mawaziri wawili wa serikali ya siasa kali za mrengo wa kulia nchini Israel waliopendekeza kwamba vita vya Gaza vinaweza kusababisha watu wa Palestina kuishi kwenye makaazi mapya.

"Tunapinga vikali kauli zilizotolewa na mawaziri hao wawili. Hazina busara wala hazisaidii," Wizara ya Mambo ya Nje ya Ujerumani ilisema.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Ufaransa ilisema maoni ya Waziri wa Fedha wa Israel Bezalel Smotrich na Waziri wa Usalama wa Kitaifa Itamar Ben Gvir hayaonyeshi uwajibikaji na yanachochea mivutano.

**DW, VOA**

# WAWILI WASHINDA TWENDE ZETU IVORY COAST 'KI-VIP'

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Dar es Salaam, Bakari Kitenge na Edson Musingi kutoka Morogoro wametangazwa washindi wapya wa droo ndogo ya Kampeni ya Twende Zetu Ivory Coast Ki-VIP, imefahamika.

Kampeni hiyo inayolenga kuwapeleka Ivory Coast mashabiki sita kushuhudia mubashara fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), inayoendelea nchini kwa wiki ya nne sasa ikiratibiwa na Kampuni ya kubashiri ya Betika kwa kushirikiana na Tigo Pesa.

Washindi wa droo kubwa wataondoka nchini Januari 15, mwaka huu kwenda Ivory Coast kushuhudia fainali hizo zitakazofanyika kuanzia Januari 13 hadi Februari 11, mwaka huu.

Washindi hao wataishuhudia mubashara pia Timu ya Soka ya Tanzania (Taifa Stars) ambayo imefuzu fainali hizo na itacheza mechi yake ya kwanza Januari 17, mwaka huu dhidi ya Morocco hatafu itakutana na Zambia na kumaliza hatua ya makundi dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC).

Wiki hii, Musingi na Kitenge wameingia katika orodha ya washindi kwenye droo ndogo inayotoa zawadi ya luninga ya nchi 70, dishi na king'amuzi chenye kifurushi kila wiki kwa washindi wawili na fedha taslimu kila siku.

Akizungumza wakati wa kukabidhi zawadi kwa mshindi wa wiki hii, meneja biashara wa Tigo, Fabian Feliciane, alisema bado fursa za kushinda fedha taslimu kila siku na luninga nyingine kila wiki ipo.

"Unapoendelea kubashiri na Betika kupitia akaunti ya Tigopesa unajiweka katika nafasi kubwa ya kushinda zawadi mbalimbali na kuingia kwenye droo kubwa ya Twende Zetu Ivory Coast Ki-VIP," alisema Fabian.

Mmoja wa washindi hao, Musingi alisema amekuwa akibashiri mara kadhaa na kampuni hiyo.

"Nimekuwa nikishinda zawadi za pesa taslimu, leo hii (jana) nimekuwa mshindi wa luninga ni faraja kwangu," alisema.

**Naye Kitenge alisema zawadi hiyo imem wongezea 'mzuka' wa kuendelea kubashiri na Betika.**

Ofisa Habari wa Betika, Juvenalius Rugambwa, alisema ni rahisi kushinda katika kampeni hiyo ya Twende Zetu Ivory Coast Ki-VIP.

"Unachotakiwa ni kuweka pesa katika Tigopesa yako na kubeti na Betika," alisema.

Stars itashiriki AFCON kwa mara ya tatu msimu huu, baada ya ile ya 1980 huko Nigeria na mwaka 2019 ilipochezwa Misri.




Meneja Biashara wa Kampuni ya Tigo, Fabian Feliciane (kushoto), akimpongeza mmoja wa washindi wa wiki hii katika droo ndogo ya Twende Zetu Ivory Coast Ki-VIP, Edson Musingi (katikati), kutoka Morogoro. Kulia ni Ofisa Habari wa Betika, Juvenalius Rugambwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Simba Queens yaiwaza JKT

**Na Saada Akida**

BAADA ya kupata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya watani zao Yanga Princess, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Juma Mgunda, amewataka wachezaji wake kusahau matokeo ya mechi iliyopita na kuanza kufikiria mchezo ujao watakaocheza dhidi ya JKT Queens.

Mgunda alisema mechi iliyopita ilikuwa muhimu na wachezaji wake wanatakiwa kufurahia matokeo lakini isivuke mipaka na sasa wanahitaji kujipanga kuelekea mechi ijayo ambayo inatarajiwa kuwa ngumu zaidi.

Alisema malengo yao ni kupata pointi tatu ili kufikia malengo ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania.

Kocha huyo alisema kikubwa wamepata alama tatu na anawapongeza wachezaji wake na ushindi huo iwe chachu kubwa ya kujiandaa kukutana na ushindani dhidi ya mabingwa watetezi wa ligi hiyo.

"Tumemaliza hii mechi, mwisho wa mchezo huu ni mwanzo wa maandalizi ya mchezo ujao ambao tunaenda kukutana na JKT Queens, hautakuwa mchezo rahisi lakini tunaenda kucheza kwa kuwaheshimu," alisema Mgunda.

Aliongeza anaifahamua vizuri JKT Queens na wataingia kuwavaa kwa tahadhari kwa sababu mechi ya mwisho walipokutana katika Ngao ya Jamii walitokana sare na mshindi alipatikana kwa penalti.

JKT Queens itaikaribisha Simba Queens Januari 9, mwaka huu kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo ulioko Mbweni, Dar es Salaam.

# Kocha JKU SC aanika sababu iliyowaangusha

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya JKU SC imeyaaga rasmi mashindano ya Kombe la Mapinduzi mwaka huu kwa aibu baada ya kuambulia vipigo mfululizo katika michezo mitatu waliyocheza.

JKU iliyokuwa katika Kundi B pamoja na Simba, APR FC (Rwanda), na Singida Fountain Gate, ilipoteza mechi zote hizo za hatua ya makundi.

Akizungumza baada ya kichapo cha mabao 3-1 kutoka kwa APR, Kocha Mkuu JKU, Salum Ali, alisema sababu kubwa iliyofanya kutofanya vizuri katika michuano hiyo ni kutopata maandalizi mazuri na ratiba kubana.

"Ratiba ya michuano hiyo haitoi mapumziko kama inavyotakiwa katika soka kwa muda wa masaa 72 kila baada ya kumaliza mchezo mmoja," alisema kocha huyo.

Aliongeza timu yake ilikosa muunganiko wa kiuchezaji uliosababishwa na nyota wake wenye uzoefu kusajiliwa na klabu nyingine katika dirisha dogo la usajili linaloendelea na hivyo kubakia na kikosi ambacho hakina 'nguvu' ya kupambana katika michuano hiyo iliyoimarika.

# Jamhuri, Jamus FC hapatoshi Mapinduzi Cup

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Jamus FC kutoka Sudan Kusini inakabiliwa na kibarua kigumu cha kuhakikisha inatinga hatua ya robo fainali ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi kwa kuvaana na Jamhuri ikiwa ni mchezo wa mwisho wa hatua ya makundi utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Amaan Visiwani hapa.

Katika mchezo huo timu itakayofanikiwa kushinda itasonga mbele katika michuano hiyo ambayo bingwa atajinyakulia kitita cha Sh. milioni 100 kama 'best looser'.

Kocha Mkuu wa Jamus, John Alier, alisema matarajio yake ni kuhakikisha wanashinda na kusonga mbele katika michuano hiyo ingawa anaamini mchezo huo utakuwa mgumu kwa sababu wapinzani wao pia wanahitaji kupata matokeo chanya.

Alisema mchezo huo ni fainali Kwa timu zote hivyo wanahitaji kutumia akili pamoja na ufundi wa kiuchezaji ili kuhakikisha wanafanikiwa na kutimiza malengo yao ya kushiriki michuano hiyo.

Naye Kocha Mkuu ya Jamhuri, Mohamed Juma, alisema wamejipanga kuhakikisha wanapata matokeo mazuri ili wasonge mbele kwa mara ya kwanza katika michuano hiyo migumu lakini pia kupata heshima.

## ZISIKUPITE

### WAN-BISSAKA SAFI UNITED

KLABU ya Manchester United inapanga kuanza mazungumzo juu ya mkataba mpya na beki wa Timu ya Taifa ya England, Aaron Wan-Bissaka, mwenye umri wa miaka 26 mwishoni mwa msimu huu. (***Mail***)

### SALAH KUBAKIA LIVERPOOL

MSHAMBULIAJI wa Misri, Mohamed Salah, mwenye umri wa miaka 31, anakaribia kuongezewa mkataba mpya na Liverpool licha ya kutakiwa na timu za Saudi Pro League. (***Football Transfers na Anfield Watch***)

### DE BRUYNE ATAJWA SAUDIA

MFUKO wa Uwekezaji wa Umma wa Saudi Arabia (PIF) umefufua nia ya kumnunua kiungo wa kati wa Manchester City na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Kevin de Bruyne, mwenye umri wa miaka 32. (***Rudy Galetti***)

### MAATSEN ANUKIA DORTMUND

KLABU ya Borussia Dortmund inataka kumsajili beki wa kushoto wa Chelsea, Ian Maatsen, mwenye umri wa miaka 21 kwa mkopo au kwa mkataba wa kudumu. (***Telegraph***)

### DORTMUND YAMTAKA SANCHO

BORUSSIA Dortmund inamtaka winga wa Manchester United, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 23 ajiunge na timu hiyo kwa mkopo katika kambi yao ya mazoezi ya Marbella wiki ijayo. (***Sky Sports***)

### OLISE KUTUA UNITED

KLABU ya Manchester United imeonyesha nia ya kumfanya winga wa Crystal Palace, Michael Olise, mwenye umri wa miaka 22 kuwa mmoja wa wachezaji wa kwanza kusajiliwa Old Trafford. (***Standard***)

### NKETIAH KIZUNGUMKUTI

KLABU ya Crystal Palace imeonyesha nia ya kumsajili mshambuliaji wa England, Eddie Nketiah, lakini Arsenal hawatamuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 katika dirisha la Januari, ikiwa hawatapata mbadala wake. (***Ben Jacobs***)

### SANCHEZ KUMRITHI HOWE

KOCHA wa Girona, Michel Sanchez, ameibuka kama mbadala wa kocha wa Newcastle United, Eddie Howe. (***Marca***)

### BENRAHMA AGEUKA LULU

KLABU ya Ligue 1 ya Ufaransa, Lyon inataka kumsajili winga wa West Ham na Algeria, Said Benrahma, huku Wolves na Fulham pia wakimtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28. (***Footmercato***)

### WERNER AKARIBIA UNITED

MSHAMBULIAJI wa Ujerumani, Timo Werner, mwenye umri wa miaka 27 amekuwa shabaha ya Manchester United, huku RB Leipzig ikitarajiwa kuruhusu mkataba wa mkopo. (***Mirror***)

### EVERTON KUMUUZA GOMES

KLABU ya Everton inatafuta kumuuza kiungo wa kati Mreno, Andre Gomes, kwa sababu ya mshahara mkubwa wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30. (***Football Transfers***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE : SIJAAMUA HATIMA YANGU PSG

**Mshambuliaji huyo aweka wazi utulivu wa klabu ni...**

**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappe amesema bado hajaamua kama atasaini mkataba mpya wa kubakia Paris Saint-Germain zaidi ya msimu huu au ataondoka kwa uhamisho wa bure msimu wa joto.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia na Ufaransa, ambaye amekuwa akilengwa na Real Madrid kwa muda mrefu, alisema msimu uliopita wa joto hakuwa na nia ya kuongeza mkataba na mabingwa hao wa Ligue 1, akimaanisha sasa ana uwezo wa kufanya mazungumzo na klabu nyingine ili kuhamia mwisho wa msimu.

**Hata hivyo, akizungumza baada ya kufunga bao na kuisaidia PSG kubeba Kombe la Ufaransa hapo juzi, Mbappe alisema akili yake bado haijakamilika.**

"Hapana, kwa kuanzia nimehamasishwa sana kufikia mwaka huu," aliwaambia waandishi wa habari baada ya ushindi wa 2-0 dhidi ya Toulouse.

"Ni muhimu sana. Tuna mataji ya kushinda na tayari tumeshinda moja.

"Bado sijafanya uamuzi, sijafanya chaguo, kwa makubaliano niliyofanya na rais wakati wa joto, uamuzi wangu sio muhimu kwani tuliweza kulinda pande zote na kulinda utulivu wa klabu."

Kama sehemu ya makubaliano yaliyofikiwa msimu wa joto uliopita, wakati klabu ilitishia lazima asaini mkataba mpya au kuhamishwa kabla ya kuanza kwa msimu huu, iliripotiwa Mbappé' alikubali kuondoa malipo ya bonasi ya uaminifu ya hadi euro milioni 100m ili aweze kuondoka bure.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 pia alikuwa karibu kujiunga na Real Madrid bila malipo msimu wa joto wa 2022 kabla ya kutangaza kwa mshtuko anabakia hapo Parc des Princes.

Alipoulizwa kama anaweza kufanya uamuzi mwingine wa kuchelewa wakati huu, Mbappé alijibu: "Sijui. Ilikuwa mwishoni mwa Mei mwaka, 2022 kwa sababu sikujua hadi Mei.

"Kama najua ninachotaka kufanya, kwa nini nisubiri? Haitakuwa na maana lakini kama nilivyosema, muhimu zaidi ni mataji. Tumeshinda moja tayari na tumedhamiria kushinda zaidi. Hali yangu binafsi ndani ya klabu, hakuna anayeizungumzia, haipendezi sana."

Mbappé, aliyesajiliwa kutoka Monaco mwaka 2017, ndiye mfungaji bora wa muda wote wa PSG na ameshinda mataji matano ya Ligue 1 akiwa na klabu hiyo.

PSG wanaongoza msimamo wa Ligue 1 kwa pointi tano na watamenyana na Real Sociedad katika hatua ya 16 bora ya Ligi ya Mabingwa. Ulaua

# ONANA AKUBALIWA KUCHELEWA AFCON

**MANCHESTER,** England

ANDRE Onana anatarajiwa kupatikana kwa mechi ya Ligi Kuu England wakati Manchester United itakapoivaa Tottenham Hotspur baada ya kufikia makubaliano na Shirikisho la Soka la Cameroon, kutokana na kuchelewa kuitwa kwake kabla ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), kwa mujibu wa ESPN.

Onana amepewa ruhusa ya kusalia Manchester kwa mechi ya raundi ya tatu ya Kombe la FA dhidi ya Wigan Athletic itakayochezwa Jumatatu na watakapoikaribisha Spurs kwenye Uwanja wa Old Trafford Januari 14, mwaka huu.

Cameroon wanaanza kampeni yao ya AFCON dhidi ya Guinea saa 24 tu baadaye Januari 15, mwaka huu.

Klabu za Ligi Kuu England vilipewa muda hadi Januari Mosi kuwaachia wachezaji wao kabla ya michuano hiyo itakayofanyika Ivory Coast kuanzia Januari 13, mwaka huu lakini United na Cameroon wamekubaliana kumchelewesha Onana.

Onana alirejea Manchester juzi baada ya kukaa kwa muda jijini Paris kufuatia kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Nottingham Forest Jumamosi iliyopita.

Kikosi cha Cameroon kwa sasa kinaendelea na mazoezi katika kambi yake iliyoko Saudi Arabia, ambapo wanatarajiwa kucheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Zambia Januari 9, mwaka huu.

Onana, kulingana na chanzo, ameonyesha nia ya kupunguza muda wake nje ya United baada ya kuiambia klabu wakati wa mazungumzo ya uhamisho wa majira ya joto amestaafu soka la kimataifa.

Kipa huyo aliachwa wakati wa fainali za Kombe la Dunia la 2022 nchini Qatar baada ya kutofautiana na Kocha, Rigobert Song, lakini akashawishiwa kurejea kabla ya mechi ya mwisho ya kufuzu AFCON dhidi ya Burundi hapo Septemba, mwaka jana.



# Neville awafunda nyota Liverpool

**LIVERPOOL,** England

NAHODHA na mlinzi wa zamani wa Manchester United, Gary Neville, amewataka wachezaji wa Liverpool kuhakikisha wanapambana kubaki katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu England baada ya kuondoka kwa Mohamed Salah.

Salah alifunga mara mbili na kutengeneza bao lingine wakati Liverpool ilipoilaza Newcastle mabao 4-2 mapema wiki hii na sasa ameondoka kwenda katika michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), akiwa na timu ya Taifa ya Misri.

Michuano ya 34 ya AFCON inatarajia kufanyika kuanzia Januari 13 hadi Februari 11, mwaka huu nchini Ivory Coast.

Wekundu hao wapokileleni kwa tofauti ya pointi tatu katika msimamo wa Ligi Kuu England, baada ya juzi kushinda na wana pengo la pointi tano dhidi ya Manchester City, ambao wana mchezo mmoja mkononi, na Arsenal, hizi ndizo timu pinzani kwenye vita ya ubingwa.



Salah amekuwa na mchango mkubwa katika mbio za Liverpool hadi kileleni mwa msimamo, akiwa amefunga mabao 14 na asisti nane katika michezo 20 aliyocheza msimu huu.

Lakini sasa shinikizo ni kwa washambuliaji wenzake ,Darwin Nunez, Diogo Jota na Cody Gakpo kuchukua mikoba ya Salah pindi atakapokuwa katika majukumu yake ya kitaifa. Watatu hao wana mabao 13 pekee kwenye ligi.

Neville alisema Liverpool wana wachezaji watatu wa viwango vya juu ambao ni Alisson, Virgil van Dijk na Salah.

"Van Dijk amerejea katika kiwango bora katika mwezi huu au miwili iliyopita. Rekodi ya safu ya ulinzi ya Liverpool imekuwa nzuri na wamepiga pasi nyingi safi. Alisson ndiye golikipa bora zaidi duniani.

"Kuna mshtuko katika theluthi ya sehemu ya mwisho inaweza kuharibika kidogo. Unajiuliza itakuwaje bila Salah?

"Bado wako kileleni mwa ligi na ni lazima wapambane ili waweze kumpa Salah nafasi ya kurejea na kuwa na mafanikio ya kweli kwenye ubingwa," alisema Neville.

# Barca yasajili straika chipukizi

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA imemsajili mchezaji mpya Vitor Roque mwenye umri wa miaka 18 kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga, kwa wakati na jana Alhamisi alitarajiwa kucheza mechi yake ya kwanza dhidi ya Las Palmas.

Barca walipata uhamisho wa Roque kutoka Athletico Paranaense Julai, mwaka jana kwa mkataba wa thamani ya zaidi ya euro milioni 60.

Kuwasili kwake Hispania hakukupangwa hadi mwanzoni mwa msimu wa 2024/25 huku kukiwa na vizuizi vya matumizi, lakini muda huo ulirudisha nyuma Januari hii.

Roque alitambulishwa na klabu yake mpya Desemba mwishoni, lakini uvumi mapema wiki hii ulidai Barca inaweza kusajili uhamisho huo na LaLiga.

Xavi alionyesha matumaini alipozungumza na vyombo vya habari juzi jioni huku usajili huo ukipewa mwanga wa kijani saa chache baadaye.

Roque alitumia msimu wa 2023 akiwa na klabu yake ya nchini Brazil akicheza kama 'namba tisa' kwa Athletico, akifunga mabao 21 katika mashindano yote.

Lakini imezua shaka juu ya jukumu atakalokuwa nalo Hispania ikizingatiwa straika, Robert Lewandowski yupo na anatumika katika mfumo wa 4-3-3.

Lakini Xavi anaonekana kujiamini wawili hao wanaweza kucheza pamoja, akitoa wito kwa Roque kuwa na uwezo wa kucheza kama mshambuliaji mpana na kutoa ushindani kwa washambuliaji wote kwenye kikosi.

"Anaweza kucheza na (Lewandowski) kikamilifu," bosi huyo alisisitiza.

"Anaweza kucheza nje au kama namba tisa. Atazalisha ushindani kwa washambuliaji wote katika kikosi - Lewandowski, Ferran (Torres), Joao (Felix), Raphinha na Lamine (Yamal).

"Tutashughulikia mambo yake hatua kwa hatua. Yeye ni mtoto mwenye umri wa miaka 18, kwa hivyo hatuwezi kumpa jukumu kwa sasa kwa sababu anahitaji muda wa kuzoea.

"Lakini yuko tayari kucheza na kufanya mazoezi vizuri. Ni mtaalamu na haraka kukabiliana na mazingira yake mapya, lakini tutakuwa waangalifu."



## HABARI MICHEZO

# MAJALIWA MGENI RASMI HARAMBEE STARS, TWIGA

**Na Saada Akida**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ataongoza hafla ya kuchangia fedha Timu za Soka za Taifa (Taifa Stars na Twiga Stars), ambazo zimefuzu kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON na WAFCON) zinazotarajia kufanyika baadaye mwaka huu.

Tayari kikosi cha Stars kipo Misri kikifanya maandalizi ya kuelekea AFCON itakayofanyika kuanzia Januari 13, mwaka huu nchini Ivory Coast.

Akizungumza na Nipashe jana, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Damas Ndumbaro, alisema katika hafla hiyo itakayofanyika Januari 10, mwaka huu kwenye Ukumbi wa Hoteli ya Johari Rotana, Majaliwa atamwakilisha Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Ndumbaro alisema ni bahati kubwa kwa timu zote mbili kufuzu fainali hizo, hivyo mipango ya kuhakikisha zinapeperusha vyema bendera nchi itanakiwa kuimarishwa.


"Lengo kubwa la harambee hii ni wadau wa soka kujitokeza kutoa sapoti kwa timu zetu kuendelea kufanya vizuri katika fainali hizo, tunaimani kubwa na makocha na wachezaji kutufikisha katika malengo yetu," alisema Ndumbaro.

Waziri huyo pia alitangaza Kamati Maalum kwa ajili ya hamasa kwa timu za Taifa zilizofuzu mashindano mbalimbali ya kimataifa ambayo inaundwa na wajumbe 16.

Alisema kamati hiyo itakuwa na jukumu la kuhamasisha mashabiki na wapenzi wa michezo ndani na nje ya nchi kujitokeza kuzishangilia na kuziunga mkono Timu za Taifa pamoja na kuratibu mambo mbalimbali.

Alimtaja Mwenyekiti ni Theobald Sabi, Patric Kahemele (Makamu Mwenyekiti), Neema Msitha (Katibu) na wajumbe wake ni Beatrice Singano, Michael Nchimbi, Jemedari Said, Nick Reynolds (Bongo Zozo), Hamis Ali, Christina Mosha (Seven), Hersi Said , Salum Abdallah (Try Again), Paulo Makanza, Mohamed Soloka, Hassan Mohamed Raza, Lucas Mhavile (Joti), Oscar Oscar (Mzee wa Kaliua), Prisca Kishamba, Burton Mwemba (Mwijaku) na Clayton Chipondo (Baba Levo).

Stars itaanza kutupa karata yake ya kwanza AFCON Januari 17 kwa kucheza dhidi ya Morocco halafu Januari 21 itaivaa Zambia na Januari 24, mwaka huu itapambana na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).




Mchopa Mgaya (katikati), akikabidhiwa mfano wa hundi ya Sh. milioni 18 na wachezaji wa Yanga, Kibwana Shomari (kushoto) na Skudu baada ya kushinda bonus kutoka SportPesa kwa kubashiri kwa usahihi baadhi ya mechi za Jackpot. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kapombe apongeza kiungo Singida

**Na Faustine Feliciane,**
ZANZIBAR

BEKI na nahodha msaidizi wa Simba katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi yanayoendelea visiwani hapa, Shomari Kapombe, amesema Singida Fountain Gate walicheza vizuri na kuwabana zaidi katika eneo la kiungo wakati timu hizo zilipokutana juzi.

Kapombe alisema katika mechi hiyo Simba ilizidiwa kika nafasi ya kiungo ukilinganisha na wapinzani wao lakini Kocha Mkuu, Abdelhak Benchikha, alibaini na kuwapa mbinu nyingine walipokwenda mapumziko.

Alisema mbinu tofauti walizopata ziliwasaidia watawale mchezo na kupata ushindi wa mabao 2-0.

"Mchezo ulikuwa mgumu sana, kipindi cha pili kocha alitupa maelekezo mengine hasa kwa wachezaji wa safu ya kiungo, na kweli tulivyoyafuata timu ilibadilika, tukaushika mchezo na kupelekea kupata matokeo haya," alisema Kapombe.

Aliongeza ushindi huo ulikuwa muhimu sana kwao kuelekea kutimiza malengo yao katika michuano hiyo kwa mwaka huu.

"Nia yetu ni kuchukua ubingwa wa mwaka huu, sasa kama tunataka kufikia huko lazima tushinde michezo yetu, hasa kuzishinda timu kubwa..., tunaamini tutafikia malengo yetu," Kapombe alisema.

Kuhusu ugumu wa ratiba ya michuano hiyo, Kapombe alisema wanakabiliana nayo kwa sababu wanafahamu mashindano hayo ni maalum na yamepangwa muda maalum.

Simba yenye pointi sita sawa na Singida Fountain Gate itashuka tena dimbani leo kuwakaribisha APR kutoka Rwanda ili kufahamu timu itakayoongoza kundi lao wakatu JKU imeshaondolewa kwenye michuano hiyo.

## Benchikha kicheko kiwango Simba SC

INATOKA UK 24

amefurahia kushiriki mashindano hayo kwa sababu yamemsaidia kupata muda wa kujwenga wachezaji wake lakini pia wale ambao hawakupata nafasi katika mechi zilizotangulia, wamepata nafasi hiyo sasa.

Aliongeza baaada ya kumaliza michezo ya hatua ya makundi, kikosi chake kitaingia dimbani katika hatua ya robo fainali kikiwa na mbinu tofauti kwa sababu wanaingia kwenye mfumo wa mtoano.

"Hatua ya robo fainali ni ya mtoano, ukifungwa katika mchezo unakuwa umetolewa nje ya mashindano hayo. Hii hatua tutakuwa na 'approach' tofauti kwa sababu ni mtoano, hatua hii lazima tucheze kwa umakini na malengo zaidi, ni hatua ambayo kosa moja litakugharimu, hivyo hata mbinu zake katika kila mchezo ni tofauti," alisema Benchikha.

Simba ikishinda mchezo wa leo itafikisha pointi tisa na hivyo kumaliza katika uongozi katika kundi lake kwa kupata ushindi wa asilimia 100.

Timu nyingine ambazo tayari zimefanikiwa kusonga mbele katika michuano hiyo ni pamoja na Azam FC, Singida Fountain Gate na Yanga ambayo jana usiku ilishuka dimbani kucheza dhidi ya KVZ ya Unguja.

Fainali ya michuano hiyo inayofanyika kila mwaka itachezwa Januari 13, mwaka huu na bingwa ataondoka na kitita cha Sh. milioni 100 wakati mshindi wa pili atajinyakulia zawadi ya Sh. milioni 50.

Mlandege ya Zanzibar walitwaa ubingwa wa mashindano hayo katika michuano iliyofanyika mwaka jana.

## Mauya afunguka,

INATOKA UK 24

Mauya aliongeza.

Kiungo huyo alisema katika timu mbalimbali alizopita alikuwa anacheza nafasi nyingi tofauti, hivyo kumpa uzoefu wa kucheza kwa ufanisi.

"Mimi nilipotoka katika timu nyingine nilizocheza sikuwa nacheza nafasi moja, nilikuwa nacheza namba nane, namba sita, namba 10, kwa hiyo naamini mwalimu ameshakiona kitu kwangu kwangu, sijawahi kumwambia naweza hizo namba, kikubwa yeye anamwangalia mchezaji wake anavyocheza na ana uwezo wa kufahamu huyu naweza kumtumia kucheza nafasi hi," alisema Mauya.

Mchezaji huyo alijiunga na Yanga mwaka 2020, kabla ya kujiunga na timu hiyo aliichezea Kagera Sugar katika kipindi cha mwaka 2019 akitokea Lipuli FC ya Iringa.

Michezo

Ijumaa Januari 5, 2024
Nipashe



Onana akubaliwa kuchelewa AFCON UK. 22



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), wakifanya mazoezi nchini Misri ili kujiandaa na Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2023), zitakazofanyika Ivory Coast kuanzia Januari 13, mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Benchikha kicheko kiwango Simba SC

## ●●●Kocha huyo pia atamba wataikabili APR FC...

**Na Faustine Feliciane,**
ZANZIBAR

WAKATI leo inawakabili APR FC katika mechi ya mwisho ya hatua ya makundi kwenye mashindano ya Kombe la Mapinduzi, Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, amesema kikosi chake kinaendelea kuimarika na pia anaridhishwa na kiwango kinachoonyeshwa na wachezaji wake.

Benchikha amesema hayo baada ya kupata ushindi wa mabao 2-0 katika mechi dhidi ya Singida Fountain Gate iliyochezwa juzi usiku na kufikisha pointi sita.

Kocha huyo alisema alifurahishwa na namna wachezaji wake walivyofuata maagizo aliyowapatia wakati wa mapumziko ambayo yalisaidia kupata mabao mawili na kuibuka na ushindi katika mechi hiyo.

Alisema kutokana na ugeni wake katika soka la Tanzania mara nyingi anatumia kipindi cha kwanza kuwasoma zaidi wapinzani wake na kipindi cha pili huingiza mbinu zake kwa wachezaji baada ya kuwaona wapinzani.

Aliongeza hiyo ndio sababu Simba inaonekana kubadilika zaidi kipindi cha pili katika michezo mbalimbali ya Ligi Kuu Tanzania Bara na sasa kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi.

"Ukiangalia kuanzia mchezo wetu wa kwanza na huu wa pili timu yangu inazidi kucheza vizuri, kikosi kinaimarika zaidi, mchezo uliopita dhidi ya JKU pamoja na kushinda lakini nilisema sijaridhishwa na kiwango cha timu, lakini mchezo dhidi ya Singida nimeridhishwa, tunaendelea kufanya vizuri zaidi," alisema Benchikha.

Aliongeza wameendelea na maandalizi kwa ajili ya kukamilisha hatua ya makundi na ana matumaini wachezaji wake wataonyesha kiwango cha juu zaidi ya walichokionyesha katika michezo miwili iliyopita.

"Sasa tunaelekea katika mchezo wetu wa mwisho wa hatua ya makundi, lengo letu tunataka kumaliza hatua hii tukiwa tumeshinda michezo yetu yote, ushindi utatupa morali kubwa kuelekea kwenye mchezo wa hatua ya robo fainali," alisema Benchikha.

Kocha huyo pia alisema

INAENDELEA UK 23

# Mauya afunguka, Yanga SC ikitoa dozi

**Na Adam Fungamwango**

MCHEZAJI wa Yanga, Zawadi Mauya, amefurahishwa na kitendo cha Kocha Mkuu wa timu hiyo, Miguel Gamondi, kugundua uwezo wake wa kucheza zaidi ya nafasi moja uwanjani kwa kumpa majukumu tofauti kulingana na mahitaji ya mechi husika, imefahamika.

Katika mechi dhidi ya Jamus ya Sudan Kusini iliyochezwa juzi usiku na Yanga kuondoka na ushindi wa mabao 2-1, Mauya, alitakiwa kucheza kama beki wa kati na kuifanya kazi yake vyema akisaidiana na Gift Fred.

Akizungumza na gazeti hili, Mauya, ambaye amezoeleka akicheza nafasi ya kiungo mkabaji maarufu namba sita, alisema Gamondi amegundua anaweza pia kumtumia katika namba nyingine na akaonyesha ubora unaotakiwa.

Mauya alisema amekuwa akihama nafasi pale anapotakiwa kufanya mabadiliko baada ya kuelezwa na Gamondi.

Nyota huyo alisema kitendo cha Gamondi kumtaka acheze kama beki wa kati kiliwashangaza wadau wengi ambao hawakufahamu kama anaweza kuitendea haki namba hiyo.

"Kama wewe ni namba sita asilia basi unakuwa na uwezo kabisa wa kucheza beki wa kati, labda uwe namba nane, ambaye kazi yake ni kwenda mbele kusaidia mashambulizi na hapo hapo kurudi nyuma kumsaidia kiungo mkabaji, lakini kwangu mimi naweza kucheza nafasi nyingi sana.

Mimi ni mchezaji, siwezi kusema ngapi, mwalimu anaweza kumtumia mchezaji kwa jinsi anavyoona na mwalimu Gamondi ameniangalia na kugundua naweza, akanirudisha kucheza beki wa kati,"

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >